# Nipashe

Jumamosi Novemba 30, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580089

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Mbunge Msigwa akana kortini Chadema kuhamasisha vurugu

UKURASA 3




UKURASA 13

# Vifurushi vipya bima ya afya kaa la moto

**ACT-Wazalendo** yaibuka, yadai ni mzigo kwa Watanzania wanyonge...*Endelea ukurasa wa 2*



Lori likiwa limezama baada ya kusukumwa na maji ya mvua yaliyofurika na kupita juu ya daraja la Mto Tirina, linalounganisha wilaya za Bunda na Serengeti, mkoani Mara juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

## MAWAZIRI WAANIKA FURSA MSIMBAZI

UKURASA 3






## Aliyehitimu kwa bango kubwa Udom afunguka

UKURASA 4




**MICHEZO** MANULA AREJESHWA STARS YA CHALENJI UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Ajinyonga kwa madai kukimbiwa na mkewe

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

WATU wanne wamekufa katika matukio tofauti wilayani Nkasi mkoani Rukwa, likiwamo la mwanamume kujinyonga kwa kutumia kamba ya nailoni baada ya kugundua kuwa mke wake amemtoroka usiku na kwenda kwa mwanamume mwingine.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Justine Masejo, alisema Raphael Leonard (49) mkazi wa kijiji cha Bumanda, Kirando wilayani Nkasi, alijinyonga chumbani kwake kwa kutumia kamba ya nailoni.

Alisema katika tukio hilo lililotokea Novemba 24, majira ya saa 6:00 usiku, Leonard kabla ya kujinyonga, alikuwa amelala na mkewe lakini aliposhtuka usingizini alikuta mke wake ametoroka usiku huo na kwenda kusikojulikana akadhani amekwenda kwa mwanamume mwingine ndipo alipokasirika na kupatwa na wivu wa kimapenzi na kuamua kujinyonga.

Katika tukio la pili, lililotokea Novemba 23 majira ya saa 8:00 mchana katika kijiji cha Mwai wilayani Nkasi, Kamanda alisema watu wawili, Japhet Jelazi (25) na Peter Silunde(8) walikufa papo hapo baada ya kupigwa na radi wakiwa wamejikinga na mvua chini ya mti.

Alisema kuwa Jelazi ambaye alikuwa akilima shambani na Silunde aliyekuwa akichunga mbuzi, baada ya kuona mvua imeanza kunyesha, waliamua kukimbilia chini ya mti ili kujikinga wasilowane na mvua, ndipo radi ilipowapiga na kufariki dunia papo hapo.

Katika tukio la tatu, alisema mtoto Emiliana Kauzeni (3) alikufa maji baada ya kutumbukia kwenye dimbwi la maji yaliyokuwa yametuama nyuma ya nyumba yao kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha mkoani hapa. Alisema tukio hilo lilitokea katika kitongoji cha Milundikwa kijiji cha Nkundi.

Kwa mujibu wa kamanda, mtoto huyo alikuwa akicheza peke yake na kisha kuzunguka nyuma ya nyumba ndipo alipokwenda kwenye dimbwi la maji lililokuwa nyuma ya nyumba na kisha kutumbukia na kufa maji huku mama yake akiwa amelala ndani akijipumzisha kutokana na uchovu wa shughuli za kilimo.

Kamanda huyo alisema kutokana na matukio hayo, hakuna watu wanaoshikiliwa lakini akawahimiza wakazi wa mkoa huo kuwa waangalifu katika kipindi hiki cha mvua za masika ili kujiepusha na madhara yanayoweza kujitokeza.

# Vifurushi vipya NHIF kaa la moto

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimepinga vifurushi vipya vya bima ya afya vilivyotolewa na Mfuko wa Taifa wa Bima (NHIF), kikidai ni mwendelezo wa kuwaumiza wananchi wanyonge.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu wa chama hicho, Dorothy Semu, alipozungumza na waandishi wa habari.

Vifurushi hivyo vilizinduliwa juzi jijini Dar es Salaam na uongozi wa NHIF, ukieleza kuwa vimegawanywa katika makundi matatu yaliyopewa majina ya 'Ninajali Afya', 'Wekeza Afya' na 'Timiza Afya'.

"Mfumo wa sasa wa bima ya afya unawalenga hasa wananchi walioajiriwa katika sekta za umma na binafsi. Ni asilimia tisa tu ya Watanzania wenye vigezo vya kuingia katika mfumo wa bima.

"Na mpaka sasa, (mfuko) unahudumia wanachama 966,792 sawa na wanufaika 4,025,693 kwa mujibu wa taarifa za Mkurugenzi wa mfuko huo.

"Kwa hiyo, asilimia 91 ya nguvu za Watanzania haimo kwenye bima ya afya. NHIF imetangaza vifurushi vipya kwa maelezo kuwa itafikia watu wengi zaidi.

"Hii ni hadaa kwa wananchi. Serikali imeamua kujiweka kando kwenye wajibu wa kutoa huduma za afya kwa watu wengi hasa maskini.

"Takwimu za Hali ya Uchumi wa Taifa, zinaonyesha kuwa mwaka 2018, Watanzania milioni 41 walikuwa wagonjwa wa nje kwenye hospitali, vituo vya afya na zahanati nchi nzima.

"Hii ina maana kuwa asilimia 77 ya Watanzania waliumwa mwaka 2018, likiwa ni ongezeko la asilimia 17 la walioumwa mwaka 2017. Katika nchi ambayo raia wake wanaumwa kwa kiwango hiki, suala la afya linapaswa kuchukuliwa kwa uzito mkubwa sana," alisema.

Semu aliongeza kuwa kitendo cha serikali kujiondoa kwenye kuhudumia raia wake kwenye afya

INAENDELEA UK. 8



Spika wa Bunge, Job Ndugai (kulia), akifurahia jambo na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi, Mhandisi John Kijazi (kushoto) na Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mutungi, walipokutana katika Ofisi ya uwanja wa ndege wa jijini Dodoma jana, wakijiandaa na safari ya kikazi ya kuelekea jijini Dar es Salaam. **PICHA: BUNGE**

# Tanzania yatakiwa kuangalia upya sheria adhabu ya kifo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Tanzania imetakiwa kuangalia upya sheria zinazohusiana na hukumu za adhabu ya kifo kwa kuwa inakwenda kinyume cha katiba na kuminya uhuru wa washtakiwa.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Jaji wa Mahakama ya Haki za Binadamu ya Afrika, Sylvain Ore, wakati akitoa hukumu ya rufani ya kesi ya Ali Rajab na wenzake watano dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kesi ya mauaji ya Ali Rajab na wezake ni miongoni mwa kesi zilizosikilizwa na Mahakama ya Haki za Binadamu ya Afrika iliyoketi mjini Zanzibar. Mahakama hiyo ilisikiliza mashauri manane na saba kati ya hayo, yalitolewa uamuzi.

Shauri la kupinga adhabu ya kifo ndilo lililovutia wasikilizaji wengi katika mahakama hiyo Zanzibar kutokana na wanaharakati duniani wanataka nchi mbalimbali kuondoa adhabu ya kifo wakidai ni kinyume cha utu na ubinadamu na katiba za nchi husika.

Mlalamikaji Ali Rajab na wenzake ambao walihukumiwa adhabu ya kifo miaka 12 iliyopita, wanadai hawakupata fursa ya kutosha kusikilizwa madai yao na pia adhabu hiyo inakwenda kinyume cha haki za binadamu, madai ambayo kwa kiwango kikubwa majaji wa Afrika wamekubaliana nayo. Wenzake waliohukumiwa adhabu ya kifo ni Angaja Kazeni, Geofrey Stanley, Emmanuel Michael na Julius Michael. Kwa sasa tayari wametumikia adhabu hiyo miaka minane jela. Katika hukumu iliyosomwa kwa zaidi ya dakika 45, huku mahakama hiyo ikiendesha kesi zake kwa mara ya kwanza Zanzibar, ilitoa maelekezo kwa serikali ya Tanzania kuangalia upya sheria inayotumika kutoa adhabu ya kifo kutokana na kile ilichosema inakwenda kinyume cha itifaki na mikataba ya kimataifa na Afrika. Pia mahakama ilisema haitoi uhuru kwa majaji kuamua aina ya adhabu mbadala.

Pia mahakama hiyo iliielekeza serikali kutoa Sh. millioni nne kwa wakata rufani kila mmoja kutokana na usumbufu walioupata kwa muda wote waliokuwa jela na ikiwa ni njia mojawapo ya kuwapoza kutokana na maumivu na madhara waliyopitia katika kipindi cha miaka 12 wakiwa jela.

Kesi tano kati ya nane ambazo zimewasilishwa kwa mahakama hiyo na kutolewa hukumu zinahusu serikali ya Tanzania na zingine ni Benin, Ghana na Rwanda.

Uamuzi wa mahakama hiyo wa adhabu ya kifo unakuja wakati dunia ikitarajia kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Kupinga Adhabu ya Kifo Desemba 10, suala la kufutwa kwa adhabu ya kifo ni moja ya hoja zinazotolewa na wananchi kwa lengo la kuimarisha utawala bora na haki za binadamu.

## HABARI KITAIFA



Mwenyekiti wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Hassan Mitawi, akifungua Mkutano Mkuu wa 21 wa Wanachama wa baraza hilo, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga.
**PICHA: MIRAJI MSALA**

# Msigwa akana Chadema kuhamasisha vurugu

**Na Hellen Mwango**

SHAHIDI wa pili wa utetezi katika kesi ya uchochezi, Mbunge wa Iringa Mjini (Chadema), Peter Msigwa, amedai mahakamani kwamba chama chake kilitumia lugha ya picha katika mikutano ya kampeni ili kuhamasisha kukichagua.

Kadhalika, amedai kuwa tuhuma zinazomkabili katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, hazina ukweli bali zimetokana na kutoeleweka lugha za kisiasa kati ya Chadema na Jamhuri.

Msigwa alitoa madai hayo jana wakati akitoa ushahidi wa utetezi wake mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, anayeskiliza kesi hiyo.

"Mheshimiwa hakimu, chama changu kilitumia lugha ya picha katika mikutano yetu ya kampeni kwa lengo la kuhamasisha watu kukipigia kura katika uchaguzi mdogo wa ubunge katika Jimbo la Kinondoni," alidai.

"Pia mwenyekiti wetu alihamasisha watu kupiga kura ili kuongeza nguvu katika kambi ya upinzani, kuongoza mapambano ni kuonyesha wananchi masuala yanayokiukwa na kuyadai kwa mujibu wa katiba," aliongeza.

Mapema upande wa Jamhuri ukiongozwa na Mkurugenzi wa Mashtaka Msaidizi, Faraja Nchimbi, ulimhoji mshtakiwa wa kwanza, Mwenyekiti Taifa wa Chadema, Freeman Mbowe, dhidi ya utetezi wake. Mbowe alidai kuwa hajui kama kuna ibara yoyote ya katiba au sheria ya nchi inayoelekeza chama cha siasa au mtu kuchukua nchi kwa kumwaga damu, kubeba majeneza, mapanga, marungu au maandamano.

Alidai kuwa tangu awe mbunge kwa miaka 15 sasa, anailinda na kutetea katiba ya nchi miongoni mwa viapo wanavyokula wakati wa kuapishwa na kwamba ana ufahamu wa baadhi ya sheria za nchi.

Alidai moja ya majukumu yake kama mbunge ni kutunga sheria za nchi, kufanya marekebisho ya sheria na aliwahi kushiriki na kwamba nchini utaratibu wa kubadilishana uongozi ni wa mihula.

Mbowe aliendelea kudai kuwa si sera ya chama chake kuhamasisha chuki, kutembea na silaha hadharani au kuhamasisha chuki katika jamii na kuvunja sheria za nchi.

Alidai hakumbuki katika ushahidi wake aliwahi kusema kama kuna mtu alikufa kwa kupigwa na risasi katika mfululizo wa mkutano wa kufunga kampeni uliofânyika katika viwanja vya Buibui Mwananyamala hadi eneo la Mkwajuni.

Mbiwe alidai Kwamba mkutano huo ulifanyika Februari 16, mwaka jana na kwamba hakushiriki kukagua watu waliodhuria mkutano huo kujua kama walikuwa na silaha au la.

Mbali na Mbowe na Msigwa, washtakiwa wengine ni Naibu Katibu Mkuu wa Chadema Zanzibar, Salum Mwalimu; Mbunge wa Kibamba, John Mnyika; Katibu Mkuu, Vincent Mashinji; na Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya.

Wengine ni Mbunge wa Kawe, Halima Mdee; Mbunge Tarime Vijijini, John Heche, na Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko.

Washitakiwa wanakabiliwa na mashitaka 13 likiwemo la kula njama kwa madai kwamba Februari 1 na 16, mwaka jana, Dar es Salaam waliku a njama ya kutenda kosa la kufanya mkusanyiko usio halali na kukiuka tamko kutawanyika.

Pia wanadaiwa kuwa Februari 16, katika barabara ya Kawawa Kinondoni Mkwajuni washtakiwa hao wakiwa na wenzao ambao hawapo mahakamani, walikiuka tamko la kuwataka kutawanyika la ofisa wa polisi, Mrakibu Mwandamizi Gerald Ngiichi kwa kugoma kutawanyika na kupelekea uvunjifu wa amani.

Inadaiwa kugoma huko kulisababaisha hofu na hatimaye kusababisha kifo cha Akwilina Akwiline na majeruhi kwa askari wawili ambao ni Konstebo Fikiri na Koplo Rahim Msangi.

# Simbachawene, Jafo waanika fursa mradi wa Mto Msimbazi

**Na Mwandishi Wetu**

UELEWA zaidi juu ya mradi wa ujenzi wa Mto Msimbazi jijini Dar es Salaam unatakiwa kutolewa ili mradi huo ufanikiwe.

Hayo Kauli hiyo ilitolewa jana jijini na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, George Simbachawene, wakati wa kikao cha kupokea wasilisho la mpango wa fursa za uwekezaji katika bonde la mto huo na suluhisho la kudumu la mafuriko katika jiji hilo.

"Mradi huu ni muhimu sana na uchambuzi wa kina unahitajika pamoja na uelewa zaidi ili kukamilisha mradi huu, na kila mmoja anatakiwa kuona umuhimu wa mradi huu," alisema.

Katika kikao hicho, Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Seleman Jafo, alisema mradi huo ni fursa ya uwekezaji katika Jiji la Dar es Salaam na ukifanikiwa, mandhari ya jiji hilo itapendeza na kuwa kivutio cha utalii.

Kikao hicho kiliandaliwa na Simbachawene, ikiwa ni maelekezo ya Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, aliyotoa ili kutafuta suluhu ya kudumu ya mafuriko katika Jiji la Dar es Salaam na kukabiliana na madhara yanayosababishwa na mafuriko.

Mawaziri wengine walitakiwa kushiriki katika upokeaji wa wasilisho hilo ni Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Waziri wa Maji na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao waliwakilishwa na maofisa kutoka wizara zao.



# Aliyehitimu kwa bango kubwa Udom afunguka

## ■Baba yake anamiliki shule ya sekondari
## ■Awa mkurugenzi, amponza mama yake

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

ALIKUWA anasomea kijiji? Ni wa kwanza kwao kupata shahada?, Ni baadhi ya maswali ambayo wengi walihoji baada ya kuona picha ya bango kubwa la kuhitimu chuo kikuu kwa Ayubu Malambugi.

Picha ya Ayubu, mhitimu wa Shahada ya Sanaa na Elimu katika Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom) mwaka huu, ilisambaa kwa kasi kwenye mitandao ya kijamii wiki iliyopita kutokana na upekee wake.

Ilikuwa picha yenye bango kubwa liloandaliwa kwa ustadi, likiwa na maneno ya kumpongeza kwa kupata shahada hiyo Novemba 22, mwaka huu, Malambugi akiwa miongoni mwa wahitimu 5,425 wa shahada ya kwanza katika chuo hicho.

Bango hilo lilikuwa na maneno yaliyosomeka 'Hongera Ayubu N. Malambugi kwa kuhitimu na kupata shahada ya kwanza ya elimu Chuo Kikuu cha Dodoma' na limempa umaarufu kijana huyo.

**SAFARI YAKE KIELIMU**

Nipashe ilimtafuta Ayubu ili kujua safari yake kielimu na sababu ya kuwapo kwa bango hilo kwenye mahafali yake.

Anasema kidato cha kwanza hadi cha nne alisoma katika Shule ya Sekondari Airport mkoani Mbeya ambayo inamilikiwa na baba yake, Nikuswiga Malambugi.

"Nilisoma pale kwa miaka minne kuanzia mwaka 2010 hadi 2013. Nilipohitimu kidato cha nne, nilifanikiwa kufaulu na kuchaguliwa shule ya serikali kwa ajili ya kidato cha tano na sita iitwayo Kiwanja, ipo wilayani Chunya. Nilihitimu pale mwaka 2016.

"Sikupata matatizo yoyote shuleni kwa upande wa walimu na wanafunzi wenzangu, ninamshukuru Mungu nilimaliza salama, nikafanikiwa kufaulu na wakati wa kujiunga na chuo kikuu, nikachaguliwa kujiunga na Udom," anasema.

**BANGO KUBWA**

Ayubu alisema bango lililompa umaarufu mkubwa kwenye mitandao ya kijamii, lilitengenezwa na baba yake na ilikuwa zawadi ya kushtukiza kwake.

"Ilikuwa kama 'surprise' (ya kushangaza) kutoka kwa baba, wanafamilia wote waliokuja Chimwaga kwenye mahafali, japo walitoka Mbeya na mzee mpaka Dodoma kwa gari lake, hakuna aliyejua kuwa ameandaa lile bango kubwa," anasema.

Ayubu anadai baba yake ni mbunifu na mara nyingi huwa si rahisi kuelewa kitu anachoandaa hadi kinapokamilika.

"Hili bango nilipewa baada ya kutoka ukumbini Chimwaga kwenye sherehe za kutunukiwa, baba akatuambia wote tulipofika nje kuwa ameniandalia 'surprise'.

"Tulipofika karibu na gari lake, akatusimamisha halafu yeye akaenda kuchukua hilo bango ikawa 'surprise' kweli kweli kwa wote tuliokuwapo, tukafurahi na tukaanza kupiga nalo picha," anasema.

Mhitimu huyo anasema alifurahi na kufarijika kutokana na ubunifu wa baba yake, akieleza kuwa imempa motisha ya kufanya vizuri zaidi katika mipango yake kimaisha.

"Nilijisikia vizuri sana na tulifurahi pamoja pale familia nzima kwa sababu najua baba yangu ni 'creative' kinoma kwa mambo anayofanya," anasifu.




Ayubu Malambugi akipozi kwa picha katika mahafali.

Ayubu anabainisha kuwa sasa anakumbana na utani mwingi hasa kwenye mitandao ya kijamii kutokana na kubamba kwa bango lake hilo.

"Mimi nauchukulia poa, mpaka rafiki zangu kwa sasa wananiita 'bango kubwa'.

"Baada ya kurudi nyumbani Mbeya, familia ilirudi Jumamosi, mimi nilirudi Jumatatu, baba akaniambia kuwa hakutarajia na hakufikiri suala hilo lingekuwa kubwa na kusambaa kwa kiwango kikubwa kwenye mitandao ya kijamii.

"Mimi kwa kweli sikutegemea, nilipatwa na mshangao mkubwa, niliona ni kitu cha kipekee sana mzee kafanya. Ndani ya zile sekunde za kwanza niliwaza kweli kuwa hii watu wataona kitu cha ajabu sana.

"Lakini, katika maisha yangu, sijawahi kuwaza ya walimwengu watasema nini, mimi nilipokea kwa furaha sana kutoka kwa baba na tulicheka sana," anasema.

**APEWA UKURUGENZI**

Ayubu anaeleza kuwa baada ya kuhitimu, ameungana na baba yake kusaidia utekelezaji wa majukumu ya uendeshaji wa shule na amepewa nafasi ya kuwa msaidizi wake, akiitwa mkurugenzi mdogo.

"Mimi ni mtoto wa tano kwa baba, walio juu yangu wawili wameajiriwa serikalini, tofauti na wengine wanavyotafsiri lile bango kwenye mitandao wakidhani labda mimi ndiyo mhitimu wa kwanza kwenye familia yetu, wapo wasomi wengine," anasema.

"Jambo la kuumiza ni kwamba, baba yangu ni mkali sana. Wiki moja kabla ya mahafali, aliniambia ninyoe ndevu maana nilikuwa nimeachia ndevu, zikawa nyingi. Sasa baba hapendi mtu afuge nywele na ndevu, yeye anaona ni uchafu.

"Sasa, mimi aliponiambia ninyoe ndevu nikamwambia nitanyoa mahafali ikipita, nikawa nimemchokoza, akasema hata mahafali yangu hatahudhuria, niliomba msamaha akakataa.

"Mama akanisaidia lakini akaambia 'wewe hujamfunza adabu', kitendo kile kiliniuma sana, lakini baadaye alinisamehe kwa sababu si unajua mtoto ni mtoto tu," anasema.

Ayubu anakiri kufanikiwa kwake kitaaluma kumetokana na usimamizi mzuri wa wazazi wake, akishauri wazazi kuwajengea msingi mzuri watoto wao kielimu kwa kuhakikisha wanafuatilia maendeleo ya watoto taaluma badala ya kuacha jukumu hilo kwa walimu.

**NDOTO YAKE**

Anasema licha ya baba yake kujikita katika taaluma anakomsaidia, ndoto yake ni kuwa mfanyabiashara mkubwa nchini.

"Malengo yangu ni kuwa mfanyabiashara. Niwe na miradi mbalimbali ambayo itaniingizia fedha nyingi huku nikiendelea kupiga kazi na baba hapa Airport High School Mbeya," anasema.

**MARAFIKI WANENA**

Kiongozi wa darasa alilokuwa anasoma Ayubu, Ismail Haji, anasema kijana huyo alikuwa anafahamika kwa mambo mawili, mwanamichezo na mtu aliyekuwa akishiriki vyema kwenye majadiliano ya masomo na wenzake.

"Ayubu alikuwa kocha msaidizi wa kikosi chetu na tulifanikiwa kuchukua ubingwa kwenye idara yenu ya Arts Media and Designing.

"Nilipoona lile bango, nilikuwa nataka kujua ni nani aliyempatia au alitengeneza mwenyewe maana ni mcheshi sana,"

INAENDELEA UK. 7

## Abiria wanusurika gari kuungua moto

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

ZAIDI ya abiria 10 waliokuwa wakisafiri kutoka Shinyanga mjini kwenda Kishapu, wamenusurika kifo baada ya gari aina ya Toyota Haice, waliyokuwa wakisafiria lenye namba za usajili T 998 AAP kuwaka moto katika eneo la Stand iliyoko soko kuu mjini hapa.

Tukio la kuwaka moto gari hilo lilitokea jana majira ya saa 8:00 mchana lilipokaribia kutoka kwenye eneo la Stand.

Gari hilo gafla lilianza kuwaka moto ndipo abiria waliposhuka na wengine wakichoropokea madirisha na hakuna aliyeungua wala majeruhi.

Akisimulia tukio hilo, mmoja wa mashuhuda, Baraka Magelegele, ambaye ni konda wa stendi hiyo, alisema wakati gari hilo likijiandaa kutoka likiwa na abiria ndani, ghafla walishangaa kusikia kishindo kikubwa na kuanza kuwaka moto, hivyo kuanza kuwatoa abiria ndani na kufanikiwa kuwaokoa.

"Gari hili wakati likijiandaa kutoka hapa stendi, likiwa na abiria ndani, ghafla tulisikia kishindo na kuanza kuwaka moto, ndipo tukaanza kuwa okoa abiria ili wasiteketee na moto. Tulifanikiwa kuwatoa wakiwa salama, huku Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilifika na kuuzima moto huo," alisema Magelagela.

Dereva wa gari hilo, Basu Gereja, alisema chanzo cha moto huo ni kupasuka kwa betri na kuungua. Alisema anamshukuru Mungu kwa kuwa hakuna mtu yeyote aliyepata madhara kwenye tukio hilo.

Kwa upande wake, Mrakibu Msaidizi wa Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Shinyanga, Edward Lukuba, alisema baada ya kupata taarifa ya gari hilo kuwaka moto, walifika na kuuzima, huku akibainisha hakuna kifo wala majeruhi.

# Mwongozo wanaonyanyasa wanawake waandaliwa

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WANAUME ambao wamekuwa wakidhalilisha wanawake sokoni kwa kuwafanyia ukatili wa kijinsia, ikiwamo kuwatolea lugha chafu za matusi ya nguoni, kuwataka kimapenzi kwa nguvu, kuwashika maumbile bila ya ridhaa, watakiona cha mtema kuni.

Hatua hiyo inatokana na watu hao kuandaliwa mwongozo wa faini au kusimamishwa kufanyabiashara kwa muda.

Mwongozo huo uliandaliwa juzi mjini Shinyanga kwa kukutanisha wenyeviti wa masoko sita ya mjini humo, maofisa ustawi wa jamii, maendeleo, polisi, wanasheria na wajumbe wa mpango mkakati wa serikali kitaifa wa kupunguza ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto (Mtakuwwa).

Ofisa Mradi wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia Sokoni, Helena Daudi, kutoka Shirika la Agape mkoani Shinyanga, alisema wameamua kushirikisha wadau hao ili watengeneze mwongozo ambao utatumika kuzuia ukatili sokoni.

Alisema katika mradi wao ambao wanautekeleza wa "Mpe Riziki Si Matusi" wa kutokomeza ukatili wa kijinsia kwenye masoko sita ya Shinyanga Mjini ambayo ni Kambarage, Soko kuu, Nguzonane, Ngokolo, Majengo Mapya na Ibinzamata, wamegundua hayana mwongozo wa kitaalamu ambao unawalinda na kuzuia vitendo vya ukatili wa kijinsia.

"Shirika letu la Agape katika kutekeleza mradi wa 'Mpe Riziki Si Matusi', tunalenga kutokomeza ukatili wa kijinsia sokoni dhidi ya wanawake na wasichana.

Tumegundua hakuna mwongozo ambao umepitiwa kisheria wa kuzuia ukatili wa kijinsia ndiyo maana tukaamua tuutengeneze ili uanze kutumika," alisema Daudi.

"Mwongozo huu utakuwa na utoaji wa adhabu kali kwa wale ambao watakuwa wakidhalilisha wanawake sokoni kwa kuwafanyia vitendo vya ukatili wa kijinsia. Kutakuwa na utozwaji wa faini mbalimbali kulingana na kosa husika na mhusika akiendelea kufanya vitendo hivyo, atafungiwa kutofanya biashara kwa muda," aliongeza.

Naye Mwanasheria wa Serikali kutoka Ofisi ya Mkurugenzi Manispaa ya Shinyanga, Mushi Josephat, alisema vitendo vyote vya ukatili wa kijinsia ni makosa ya jinai na kubainisha mwongozo huo utasaidia kuonyana na mtu akipelekwa mahakamani ni kifugo au kulipa faini au vyote kwa pamoja.

Mwenyekiti wa Soko Kuu la Shinyanga Mjini, Alex Stephen, alisema mwongozo huo utasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza ukatili sokoni na utakuwa umepitiwa na wanasheria na watautumia vyema kuwabana wale ambao wanadhalilisha wanawake.



Dereva wa Bodaboda akiangalia chombo chake baada ya kubanwa na Daladala, wakati akitaka kupenya katikati ya magari, katika eneo la Mabibo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Majaliwa asema madhehebu chimbuko la viongozi bora

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amesema madhehebu ya dini yametoa mchango mkubwa katika kuwapata viongozi wa serikali wanaofuata maadili mema na miiko ya uongozi.

Akizungumza wakati alipofungua Msikiti wa Haq - Kionga ulioko Magomeni, jijini Dar es Salaam jana mchana, Majaliwa alisema imedhihirika kwamba waumini wazuri wa dini mbalimbali wamebainika kuwa ni viongozi wazuri na waadilifu ndani ya serikali.

Majaliwa aliwasihi viongozi wa dini kuendelea kuwafundisha maadili mema waumini wao ili taifa liendelee kuwa na raia wema ambao baadhi yao ndio watakaokuwa viongozi katika ngazi mbalimbali baadaye.

"Nyumba za ibada ndiyo mahali sahihi panapojengwa maadili mema kwa watu wa rika zote, hivyo nawaomba WA Tanzania wawe waumini wazuri wa dini zao kwani kwa kufanya hivyo watakuwa pia raia wema," alisema.

Alisema wazazi na walezi wanawajibika kuwarithisha watoto wao imani za dini vizuri kwa kuwa anaamini kwa kufanya hivyo, watoto watajengewa misingi mizuri ya imani ya dini na maadili mema na watakapokuwa watu wazima watakuwa raia wema.

Majaliwa aliwasilisha mchango wa Rais John Magufuli wa Sh. milioni 10 na yeye pia alichangia Sh. milioni tano ili zisaidie katika awamu ya pili ujenzi wa msikiti huo.

Naye Sheikh Masoud Jongo ambaye alimwakilisha Sheikh Mkuu wa Tanzania katika ufunguzi wa msikiti huo, alisema uhuru mkubwa wa kuabudu uliopo nchini ndiyo sababu kubwa inayoifanya Tanzania iwe ni nchi ya amani na utulivu.

Sheikh Jongo amewaomba Watanzania wautumie vizuri uhuru mkubwa wa kuabudu uliopo nchini kwani ni nchi chache duniani zinazotoa uhuru mkubwa wa kuabudu kwa wananchi wake kama ilivyo hapa Tanzania.

Baadhi ya viongozi walioshiriki katika ufunguzi wa msikiti huo ni Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Hussein Mwinyi; Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega; Mbunge wa Mtwara Vijijini, Hawa Ghasia na Mbunge wa Kibaha Vijijini, Abuu Juma.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Tanzania tunahitaji Mwakinyo wengine

**WAKATI** jana usiku, bondia wa ngumi za kulipwa nchini, Hassan Mwakinyo, alikuwa anapanda jukwaani kupambana na mpinzani wake, Arnel Tinampay, kutoka Filipino, huu ni wakati mwingine wa kukumbuka kuzalisha mabondia wengine.

Mwakinyo anaonekana kufanya vizuri baada ya kupata udhamini kutoka katika kampuni mojawapo ya michezo ya kubahatisha hapa nchini.

Kwa muda mrefu, Tanzania ilikuwa imepotea kwenye medani na ushindani wa kimataifa katika mchezo wa ngumi, lakini kupitia bondia huyo kutoka jijini Tanga, tumeanza kupeperusha bendera yetu.

Hata hivyo, Mwakinyo, ambaye kwa Afrika anashikilia nafasi ya kwanza, kama walivyo wanamichezo wengine ambao wanafanya vema kimataifa, amepata umaarufu kutokana na jitihada zake binafsi.

Bondia huyo alianza kujifua kwa kutumia vifaa vya "mtaani", lishe ya kubahatisha, lakini leo hii Watanzania tunajivunia kutokana na nafasi ambayo amefikia katika mchezo huo.

Wadau wa michezo ambao wanaongozwa na serikali, taasisi na kampuni mbalimbali, huu ndio muda sahihi wa kuwekeza katika mchezo huo kwa kusaidia maandalizi, kuleta makocha wenye uzoefu na kuwanunulia vifaa vya kisasa mabondia chipukizi ambao wameonyesha kuwa na vipaji.

Kamwe tusisubiri mpaka Mwakinyo 'apotee", huku kutakuwa si kusaidia maendeleo ya michezo na inatakiwa kutumia jina la bondia huyo kuendesha mafunzo mbalimbali ya kuwaendeleza mabondia chipukizi kutoka mikoa yote hapa nchini.

Imetuchukua muda mrefu Watanzania kupata bondia ambaye anafanya vema katika mapambano ya kimataifa, tangu zama za Rashid Matumla 'Snake Boy" na Maneno Oswald 'Mtambo wa Gongo" kustaafu mchezo huo, wakiwa na mikanda mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ambayo waliichukua.

Nipashe tunasema kuwa, kama tunavyoshuhudia katika upande wa soka, wakati kiwango cha nahodha wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta, ambaye anacheza soka la kulipwa katika klabu ya KRC Genk inayoshiriki Ligi Kuu Ubelgiji, kikiwa bado juu, tayari wachezaji wengine wanafanya vema kwenye klabu za nje akiwamo Simon Msuva na Abdallah Yusuph.

Tunashuhudia mshambuliaji chipukizi, Kelvin John, tayari ameshafanya majaribio katika klabu mbalimbali za Ulaya, na hii inamaanisha kwamba wataungana mapema kupeperusha bendera ya Tanzania kwa kucheza soka la kulipwa sambamba na Samatta.


Hali hii ndio tunataka kuiona pia katika mchezo wa ngumi, kwa Mwakinyo, kuwavuta mabondia wengine hali ya kuwa yeye bado anafanya vema kwenye mashindano ya kimataifa anayoshiriki.

Kuandaa wanamichezo chipukizi, ndio siri pekee ambayo itatufanya Watanzania kuwa na mabondia wengi watakaokuwa wanapambana mara kwa mara na kuacha kutegemea kumuona bondia mmoja akishiriki mashindano mbalimbali.

Endapo tutafanikiwa kuwa na mabondia wengi wenye viwango vinavyofanana na Mwakinyo, inamaana bendera ya Tanzania itakuwa ikipeperushwa katika mashindano mengi zaidi, lakini pia mchezo huo ukiendelea kutoa ajira kwa vijana hao pamoja na makocha wao.

Njia hii ndio itatufanya tung'are zaidi katika medani za kimataifa, kwa sababu tunaamini mafanikio yoyote kwenye michezo, hayawezi kupatikana kwa miujiza, ila kwa kuwa na maandalizi sahihi ambayo yanaanzia katika kuwapa mafunzo mabondia chipukizi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Atangaye sana na jua hujua

Na Barnabas Maro

**KUTEMBEA** kwingi ni kujua mengi kwa kuwa mtu anaishia kukusanya maarifa mengi. Methali hii yatunasihi tutembee na kujifunza mengi.

Mpira wa miguu ni kati ya michezo inayopendwa sana duniani. Huitwa kabumbu, kandanda, soka na gozi. Ili kuupamba zaidi mchezo huo, wengine husema 'gozi la ng'ombe nyama kala nani?'

Ni mchezo wenye fadhaa yaani hali ya wasiwasi; jakamoyo. Hali ya mtu kupatwa na m-babaiko kutokana na jambo la kushtua. Mchezo huo huvuta maelfu ya watazamaji wanaojaza viwanja hasa kwa hapa nchini, zinapocheza timu mbili zenye mvutano mkubwa, Simba na Yanga. Nimeona baadhi ya wanachama au mashabiki walioahidi kutoa wake zao endapo timu zao zitashindwa! Sasa naelewa ni kwa nini wahenga walisema "Kipendacho moyo ni dawa."

Maana yake kitu anachopenda mtu au inachopenda roho ya mtu huwa ni kama dawa yake. Methali hii yaweza kutumiwa kumpigia mfano mtu anayeelekea kukipenda kitu fulani sana ingawa wengine wanakiona kuwa kibaya.

Kinachowaangusha watazamaji uwanjani na kuzirai zichezapo Simba na Yanga ni kitu gani? Ni ahadi zilizotolewa na wanachama, wapenzi na mashabiki wa timu hizo kuwa moja 'lazima' ishinde na kama ikishindwa, basi atakuwa radhi kutoa kitu alichoahidi kumpa mpinzani wake!

Baadhi ya mashabiki wa timu hizo hupandwa na mizuka (mapepo) timu zao zinaposhinda au kushindwa!

Nakumbuka miaka ya '60 pale Magomeni Mapipa palipokuwa na mzunguko, kuna shabiki wa Simba aliyekesha juu ya mti baada ya timu yake kuishinda Yanga!

Ni nadhiri aliyojiwekea endapo Simba ingeishinda Yanga na alitimiza. Kumbe ndo maana wahenga walisema: "Ahadi ni deni na deni ijuzie." Maana yake ahadi ni kama deni, mtu akitoa ahadi lazima aitimize. Methali hii yatufunza umuhimu wa kutimiza ahadi tutoazo. Ni wakati Yanga ilipokuwa ikiitesa sana Simba kila zilipokutana kwenye uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam.

Vimuyemuye (wasiwasi, wahaka) vya Simba na Yanga vilikuwepo tangu zamani. Kwenye makutano ya barabara za Mafia na Msimbazi, kabla ya timu hizo kucheza, walikuwepo wanachama wa pande zote mbili. Kila mmoja alitokosa majani kwenye chungu chake huku bendera zao zikipepea mbele. Chini kuliwekwa sinia kubwa kila upande ili wanachama na mashabiki waweke kiasi chochote cha hela. Jambo hilo lilifanyika bila kutukanana, kusukumana wala kuoneana wivu kwa upande uliokusanya fedha nyingi zaidi.

Simba ilipoishinda Yanga, kombe lilizungushwa jiji zima la Dar es Salaam hata kupita nje ya klabu ya Yanga na mashabiki kutumbukiza kiasi chochote cha hela ndani ya kombe. Kadhalika ilikuwa vivyo hivyo Yanga ilipoishinda Simba na kutwaa kombe.

Siku hizi timu hizo zachukiana mithili ya m-mbwa na paka! Hakuna yoyote inayothubutu kupita na kombe la ushindi mbele ya klabu ya mwingine. Kinachosemwa 'utani wa jadi' kimepitwa na wakati kwani sasa ni ubaya ubaya tu! Uhasama huo umesababisha hata timu ngeni inapokuja kucheza na Simba au Yanga, kupokewa na moja ya timu hizi na kuwapa siri zote za Simba au Yanga!

Kwa vile 'wajinga ndiwo waliwao," timu ngeni huja na jezi zenye rangi za Simba na Yanga, nasi kwa uzuzu (uwezo mdogo wa kufahamu mambo; hali ya mtu kutolijua jambo linaloendelea) wetu huzinunua na kuzivaa siku ya mechi huku tukizishangilia timu ngeni!

Kama Simba na Yanga ni ya Watanzania, kwa nini tufanyiane uhasama? Upendo ule wa zamani u'wapi? Kwa nini tuchukiane ili kuwafurahisha wageni? Hatujui tunajidharau na kujitukana wenyewe!?

Mbona zamani tulikuwa waungwana (watu tunaojistahi, wenye tabia inayokubalika katika jamii) lakini sasa tumekuwa watwana (wanaume wanaomilikiwa na watu wengine na kufanyishwa kazi bila ujira) wenyewe kwa wenyewe?

Siku hizi mpenzi au mwanachama wa Yanga kukaa upande wa Simba au mpenzi wa Simba kukaa upande wa Yanga atajuta kuzaliwa.

Kule kuvaa jezi ya Simba ukaonekana umekaa upande wa Yanga au kuvaa jezi ya Yanga ukaonekana upande wa Simba ni kitimbi (kitendo cha hila kinachotendwa dhidi ya mtu mwingine; kitendo cha kuchekesha au kumdhalilisha mtu)!

Nakumbuka zamani, nikiwa na mwenzangu tulikwenda kuangalia mechi ya Simba na Yanga. Kwa kuwa upande wa Yanga ulifurika pomoni (katika hali ya kujaa au kuwa -ingi) tulikwenda kukaa jukwaa la Simba.

Simba ilikuwa ya kwanza kuifunga Yanga tena kwa bao la mapema. Wenzetu wakaruka kushangilia huku sisi tukijikunyata kama tuliomwagiwa maji ya baridi sana. Mwenzangu akaniambia: "Tulia watanyamaza sasa hivi."

Baada ya muda mfupi Yanga wakasawazisha nasi tukaruka kushangilia bao lile. Dakika kumi baadaye Yanga ikafunga bao la pili na la ushindi na kutufanya turukeruke sana na kushangilia.

Ingawa tulikuwa upande wa Simba, hakuna yeyote aliyetufukuza. Ingekuwa siku hizi, tungenyanyuliwa, kutukanwa, kupigwa na kutupiwa upande wa Yanga! Kwa nini tumeuacha uungwana ule? Tujitathmini.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# Aonya viongozi mitaa kutumia nafasi zao kutafuta utajiri

**Na Tiganya VincentA**

KATIBU Tawala Mkoa wa Tabora, Msalika Makungu, amewataka viongozi wa vijiji na mitaa waliochaguliwa hivi karibu kutumia fursa hiyo kuwatumikia wananchi waliowachagua na sio kutafuta utajiri.

Amesema hatua hiyo itasaidia kuwajengea matumaini wananchi waliowachagua na ambao hawakuwachagua, hivyo kuondoa matatizo mbalimbali yanayowakabili katika maeneo yao.

Makungu alisema hayo jana wilayani Kaliua wakati wa mafunzo elekezi kwa wenyeviti wa vijiji, vitongoji na wajumbe wa Wilaya ya Kaliua, waliochaguliwa hivi karibuni na kuapishwa. "Uongozi ni dhamana na wala si nafasi ya kutumia kujitajirisha kinyume cha sheria. Waliowachagua wana imani kubwa nanyi, lakini wanazo changamoto nyingi. Nyinyi ni mashahidi kuwa rushwa bado ipo, msiende kuwa washirika wa kuwadidimiza wananchi," alisisitiza. Alisema bado kuna wananchi wanasumbuliwa na watu wenye tabia za kujitafutia mapato kwa njia zisizo halali na wengine bado wanabambikiwa kesi kwa lengo la kuwataka watoe pesa isiyo stahili jambo linalowakatisha tamaa.

Katibu Tawala huyo aliongeza kuwa wako mabinti wanapatiwa mimba wakiwa shuleni na kukatisha masomo wala hakuna hatua zinazochukuliwa na viongozi hao wa mitaa na vijiji jambo linaloonyesha udhaifu katika kutekeleza majukumu yao kama viongozi wa ulinzi katika maeneo yao. Alisema wananchi wamewachagua wakiwa na imani kuwa watalinda haki za watoto wao na haki zao pindi wanapotaka kunyanyaswa ili wawe na mazingira mazuri ya kuwa washirika wa maendeleo yanayoletwa na serikali ya awamu ya tano.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua, Dk. John Pima aliwataka viongozi walioapishwa kusaidia katika utatuzi wa migogoro katika maeneo yao na kuepuka vitendo vya rushwa.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara (kushoto), akiagana na baadhi ya wazee, baada ya kufungua mkutano wa Mtandao wa Mashirika ya Wazee Tanzania, jijini Dodoma jana, ambapo aliomba kutungwa kwa sheria ya kuwalazimisha watoto kuwatunza wazazi wao. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Azaki zapinga sheria kandamizi

**Na Enock Charles**

BAADHI ya Asasi za Kiraia (Azaki) zimeitaka serikali kuondoa vizuizi vinavyodaiwa kuwekwa kupitia sheria zilizotungwa hivi karibuni juu ya utendaji kazi wa asasi hizo.

Zimesema kuna haja serikali kuwa na mifumo rafiki utakaoziwezesha kufanya kazi kwa ufanisi. Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari kwa niaba ya asasi hizo, Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba Tanzania, Hebron Mwakagenda, alisema pamoja na jitihada za serikali kuleta maendeleo na kupambana na rushwa ni muhimu wananchi wakawa na uwezo wa kuiwajibisha serikali ili kujenga dhana ya uwajibikaji.

"Serikali yetu inajitanabaisha kuwa inapambana na rushwa lakini ukweli ni kwamba huwezi kupambana na rushwa gizani, lazima kuwe 'civic space' (nafasi za kiraia) itakayowawezesha wananchi kuiwajibisha serikali yao ambayo sisi kama asasi za kiraia tunaona imepungua kwa kiasi cha kutisha," alisema.

Mwakagenda alisema kupungua kwa nafasi za kiraia katika siasa kunaleta hali ya wasiwasi kwa maendeleo ya nchi kunakokwenda sambamba na uanzishwaji wa sheria, maagizo ya makatazo na vitisho vya baadhi ya viongozi wa serikali kwa watetezi wa haki za binadamu na wadau mbalimbali wa mashirika yasiyo ya kiserikali.

Wakili kutoka Taasisi ya Watetezi wa Haki za Binadamu, Leopord Mosha, alisema kwa kuzingatia ahadi zilizotolewa na serikali kuheshimu na kulinda haki za raia zilizowekwa kikatiba na mikataba ya kimataifa, inashangaza kwa serikali kutoa matamko na makatazo mbalimbali dhidi ya asasi hizo.

Alitolea mfano wa uchaguzi uliopita wa serikali za mitaa, akidai asasi nyingi zilinyimwa kushiriki kama waangalizi wa ndani katika uchaguzi huo na chache zilizobahatika kupata nafasi hiyo, zilicheleweshewa barua ya ruhusa ya kufanya hivyo.

"Changamoto hii tunayoiita Civic space ipo kila mahali Afrika na duniani kwa ujumla, siyo Tanzania tu, lakini kwa sasa hali ni mbaya zaidi katika nchi yetu na sisi tunaona hii si sawa, serikali inapaswa kutambua kuwa wananchi ndiyo wanapaswa kupewa uwezo wa kuwawajibisha viongozi wao," alisema.

## Aliyehitimu kwa bango kubwa Udom afunguka

INATOKA UK. 4

Haji anasema.

Anaeleza kuwa bango hilo lilimpa funzo kwamba, bado kuna wazazi wanaopenda kutoa motisha kwa watoto wao ili wafanye mambo makubwa zaidi.

"Kuna wengine wanatoa zawadi fulani kama motisha kwa mhitimu kutokana na mazingira ambayo ametoka, wengine wanatoa zawadi kama ile.

"Kimsingi, kila mtu anachukulia kwa uzito wake, mzazi wake alitaka kuonyesha umma wa Udom kwamba mzazi amefurahishwa na hatua hiyo," anasema.

Mwalimu Yohana Mwalusambo anayefundisha katika shule ya baba yake, anasema bango hilo ni motisha iliyotolewa na mzazi kwa mtoto kwa kuhitimu shahada ya kwanza.

"Hii sisi kama walimu tuliona ni suala kama motisha, yalizungumzwa mengi kuhusu picha yake, iliibua mijadala mitandaoni kwa kuwa ni nadra kufanyika kwa mhitimu wa chuo kikuu.

"Wapo waliosema anasomea kijiji, wengine wakasema ni mhitimu wa kwanza wa familia, kumbe si kweli. Bango lile ilikuwa ni kama kutambua kuwa amehitimu masomo yake,"anasema.

Andrew Malambugi ambaye ni kaka wa Ayubu, naye anakiri kushangazwa na bango la baba yao, akieleza kuwa hakutarajia kama mzee wao angeibuka na kitu hicho.

"Kiukweli, lile bango lilikuwa 'surprise' kwetu, lakini baba yenu ni mbunifu, huwa anatumia akili kubwa kufikiria kitu cha tofauti ambacho hata mtu mwingine akiona, anaanza kushangaa," anasema.

"Tulipoona jambo hilo linasambaa kwa kasi mitandaoni, tulishtuka lakini tulichukulia kawaida maana watu hawajazoea kuona bango la aina hiyo kwenye mahafali ya chuoni.

"Kuna watu walihisi Ayubu ni wa kwanza kuhitimu chuo kikuu katika familia yetu, lakini siyo kweli, Ayubu ni wa nne kwa watoto wa mzee kuhitimu chuo kikuu, wengine wawili wapo vyuo vikuu, wengine waliobaki wako sekondari na msingi. Kwa kifupi, familia yetu wote wameenda shule," alisema.

# Vifurushi vipya NHIF kaa la moto

INATOKA UK. 2

kwa kutangaza vifurushi vipya vya bima, ni kuwatenga wenye kipato cha chini.

Alisema gharama zilizowekwa katika vifurushi hivyo vipya zinajenga matabaka mawili katika utolewaji wa huduma za afya; la wenye nacho na wasio nacho.

"Binadamu hachagui kuumwa au aina ya ugonjwa ambao unapaswa kuugua, utaratibu huu wa vifurushi unachukulia kwamba suala la ugonjwa ni jambo la hiari, kwamba mtu anaweza kuchagua kuumwa ugonjwa huu ama kuukataa ule, hivyo atatibiwa kutokana na chaguo lake.

"Mtazamo wa namna hii ni hatari sana katika ujenzi wa jamii yenye utu, usawa na yenye haki. Duniani kote kuna bima aina mbili, ya binafsi na ya umma. Kiwango cha malipo ya kila mwaka kwa kila mtu ni tofauti kulingana na vigezo tofauti.

"NHIF kimsingi ni skimu ya bima ya afya ya umma, na kwa maana hiyo viwango vya malipo vinatokana na uwiano wa kipato cha mtu na mafao yanapaswa kuwa sawa kwa watu wote bila kujali kiasi cha mchango wanaotoa.

"Kitendo cha kutoa vifurushi vya malipo tofauti, na huduma kutolewa kwa kuzingatia kifurushi, ni kitendo cha kuifanya NHIF kuwa bima binafsi na 'kubidhaisha' afya ya Watanzania," alidai.

Chama hicho kilishauri kusimamishwa kwa huduma ya vifurushi hivyo vipya ili kupunguza matumizi makubwa ya rasilimali fedha.

"Kwa mfano, badala ya kuzuia wananchi wa kipato cha chini kupata huduma mbalimbali kama MRI na CT scan, serikali itoe ruzuku kwa wananchi hao kwa kuwalipia NHIF. Huu ndiyo wajibu wa serikali kutokana na kodi inazokusanya kutoka kwa wananchi," alisema.

Chama hicho pia kilitoa wito kutazamwa upya mfumo wa hifadhi ya jamii ili ndani yake kuwe na bima ya afya kwa Watanzania wote na kwamba kwa kutumia utaratibu huo, hifadhi ya jamii itasaidia wananchi kujiwekea akiba.

# Biashara mtandao yaleta mapinduzi ushindani

**Na Elizabeth Zaya**

TUME ya Ushindani wa Biashara (FCC) imesema kukua kwa biashara mtandao kumesaidia kuimarisha mifumo ya uwazi na kurahisisha shughuli za biashara nchini.

Mwenyekiti wa FCC, Profesa Humphrey Moshi, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusu maadhimisho ya Siku ya Ushindani Duniani yatakayofanyika Desemba 3 hadi 5, mwaka huu.

Prof. Moshi alisema miongoni mafanikio yaliyopatikana kutokana na biashara mtandao ni pamoja na kurahisisha miamala ya bidhaa na huduma mbalimbali kitaifa na kimataifa.

Pia alisema miamala hiyo imeongeza ubunifu kwa kampuni mbalimbali kufanya kazi kwa mfumo wa kidijitali na kuongeza ubora wa bidhaa zao.

"Kukua kwa biashara mtandao kumebadilisha mfumo wa ufanyaji biashara duniani ikilinganishwa na miaka ishirini iliyopita na imesaidia kuongeza maradufu thamani ya biashara," alisema. "Wimbi hili la biashara mtandao halikwepeki na linakuja na fursa na changamoto nyingi za kiushindani na kumlinda mlaji. Kwa upande mwingine ushindani katika nyanja ya biashara mtandao umeleta mafanikio nchini." Aliongeza.

Prof. Moshi alisema pamoja na mafanikio mbalimbali yanayotokana na biashara hiyo ya mtandao, kumekuwapo na changamoto kadhaa ikiwamo baadhi ya wafanyabiashara kutokuwa waaminifu na hata kuwatapeli wateja wao au kuwauzia bidhaa zisizowiana na matangazo wanayoweka mitandaoni.

Changamoto nyingine, alisema ni kukosekana mfumo thabiti wa kutanzua malalamiko yanayotokana na udanganyifu katika biashara hiyo au kulipwa fidia pale mteja anapouziwa bidhaa isiyokidhi matarajio.

Pia alisema changamoto nyingine ni kutokuwapo kwa utaratibu wa watumiaji bidhaa kupatiwa elimu ya haki na wajibu wao kabla ya kufanya ununuzi.



Mafundi wa wanaojenga barabara za juu za mpishano (Interchange) kwenye makutano ya Barabara ya Morogoro, Mandela na Sam Nujoma eneo la Ubungo, jijini Dar es Salaam, wakiendelea na hatua ya uwekaji lami kwenye barabara hizo, jana. Kwa mujibu wa Kampuni inayojenga ya China civil engineering construction cooperation (CCECC) ujenzi unatarajiwa kukamilika Desemba 2020. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wanafunzi wenye ualbino wasaidiwa

**Na Mary Geofrey**

SHIRIKA la Under The Same Sun (UTSS), limetoa kompyuta mpakato 20 kwa wanafunzi 20 wa mwaka wa kwanza wa ngazi ya astashahada, shahada ya kwanza na ya pili, kwa wenye ualbino kwa ajili ya kuwasaidia katika masomo yao.

Mkurugenzi Mtendaji wa UTSS, Berthasia Ladislaus, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, muda mfupi baada ya kukabidhi kompyuta hizo, alisema tangu mwaka jana wamefadhili wanafunzi 73 wenye ualbino.

"Kwa mara nyingine tena, hii ni awamu ya nne na mbele yenu ni wanavyuo 20 wakiwamo wavulana 13 na wasichana saba wenye ualbino. Leo (jana) kila mmoja amekabidhiwa kompyuta mpakato mpya zilizotolewa na shirika hili. Kompyuta hizi zimeboreshwa kwa kuwekewa herufi kubwa zaidi kuwasaidia wanafunzi wenye uoni hafifu kuona herufi zote kwa urahisi zaidi," alisema Ladislaus.

Alisema katika awamu nne za kutoa msaada huo, wameshawapa kompyuta mpakato wanafunzi 73 wanaosoma katika vyuo vikuu mbalimbali nchini pamoja na mafunzo kupitia mradi wa Vivian Grace Ash.

Mkurugenzi huyo alisema thamani ya kompyuta mpakato zilizotolewa jana ni Sh. milioni 101.9 na kwamba zitawasaidia katika nyanza ya sayansi na teknolojia ili kuunda mawasiliano, ripoti, tafiti, mafunzo kwa vitendo na kujisomea mtandaoni kwa maandishi ya kukuza.

"Tunaimani zitawasaidia katika maisha yao ya chuo ambayo yana changamoto nyingi hususani katika zama hizi za sayansi na teknolojia. Matumizi ya visaidizi hivi hayaepukiki katika kufanyia kazi mbalimbali za chuoni zinazotolewa na walimu," alisema.

Aliwataka wanafunzi wenye ualbino kusoma kwa bidii na kutumia kwa ufasaha kompyuta hizo ili kuwasaidia katika kufanya vizuri kwenye masomo yao.

Naye Ofisa wa Idara ya Elimu, Omary Mfaume, alisema mchakato wa kuwapata wanafunzi hao ulikuwa ni kuangalia wenye uhitaji ambao ni wa mwaka wa kwanza.

Naye mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Elizabeth Senkoro, alisema kompyuta hiyo itamrahisishia kufanya kazi zake kwa urahisi na ubora wa hali ya juu.



Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Mark Ocitti (wa pili kulia), akizungumza wakati wa mkutano wa Baraza la Biashara la Jumuiya ya Afrika Mashariki, jijini Arusha juzi. Wengine ni Mkurugenzi wa Ushuru na Biashara wa Sekretariati ya EAC, Kenneth Bagamuhunda (kushoto), Meneja wa Kanda wa Coca Cola, Artur Miranda na David Tarimo kutoka kampuni ya PWC. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Longido kinara ukatili wa kijinsia

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

KATIKA kuelekea kilele cha Wiki ya Kupinga Ukatili wa Kijinsia Desemba 10, mwaka huu, Wilaya ya Longido mkoani Arusha, imetajwa kuwa kinara katika matukio ya kikatili kwa watoto na wanawake.

Akizungumza juzi katika kikao kazi cha kupanga mikakati ya kukabiliana na matukio hayo, Ofisa Ustawi wa Jamii wilayani hapa, Atunagile Chisunga, alitaja matukio hayo kuwa ni ulawiti, ubakaji, ukeketaji, mimba za utotoni na vipigo kwa wanawake.

Alisema maeneo yanayoongoza kwa matukio ya ulawiti na ubakaji ni mji wa Namanga ambao umeathiriwa na matukio hayo na Kata ya Kimokouwa ambako watoto wa kike wamekuwa wakibakwa wanapokuwa machungani.

Chisunga alisema wanawake katika maeneo tofauti wilayani humo, wanapigwa na waume zao kwa makosa ya kupotea kwa mifugo na kuruhusu watoto wa kike kwenda shuleni hali ambayo ni hatari kwa afya.

"Kuna mwanamke alipigwa juzi katika Kijiji cha Lang'atadapash kisa mifugo imepotea. Aliumia sana wakaficha hali ilivyozidi kuwa mbaya ndipo wakafichua siri. Kwa kweli matukio mengi ya Longido yanafanyika kwa siri," alisema Chisunga.

Alisema wilaya hiyo inakabiliwa na mimba na ndoa za utotoni. Mwaka huu, kwa mfano, alisema watoto watatu chini ya umri wa miaka 17 walijifungua na kati yao wawili wamefariki dunia.

Chisunga alisema serikali kwa kushirikiana na wadau wameanza kujadiliana namna ya kukabiliana na matukio hayo.

Alisema sababu za kuongezeka kwa matukio hayo ni mila potofu, umaskini, imani za kishirikina, mfumo dume, ulevi, matumizi ya dawa ya kulevya, malezi mabaya kwa watoto na matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii.

"Kamati ya kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia kwa kushirikiana na wadau imeafikiana kuanzia Januari, mwakani, elimu itatolewa katika tarafa zote nne za wilaya hii," alisema.

Ofisa Jinsia Wanawake na Maendeleo ya Vijana kutoka Shirika la Maendeleo ya Jamii lisilo la kiserikali Pingo's Forum, Nailejiji Tipai, alisema shirika hilo linafanya kazi kwa kushirikiana na halmashauri mbalimbali nchini kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia.

"Hadi sasa tumeshatoa elimu ya kutoa taarifa kuhusiana na matukio ya kikatili ikiwamo ukeketaji kwa viongozi wa mila na wadau mbalimbali katika halmashauri nane zenye jamii ya watu kabila la kifugaji ambazo ni Siha, Hai, Hanang, Handeni, Ngorongoro, Korogwe, Babati na Longido," alisema Nailejij.

Alisema wamebaini wilaya zilizopo mipakani na nchi za jirani, mfano mpaka wa Namanga kati ya Tanzania na Kenya, kumekuwapo na tabia ya wazazi wa Tanzania kuwapeleka watoto wa kike upande wa Kenya kwenda kufanyiwa vitendo vya ukeketaji kwa kuhofia sheria za nchi.

# Shule zahimizwa kujenga msingi bora katika elimu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHULE za msingi na sekondari nchini, zimetakiwa kuwaandaa wanafunzi kuwa na maadili mema kwenye jamii na kuwajengea msingi bora wa kielimu ili kuwawezesha kujiajiri na kuondokana na tatizo la ajira.

Rai hiyo ilitolewa na Mkufunzi Mstaafu wa Chuo cha Diplomasia nchini, Riziki Shahari, wakati akizungumza juzi kwenye hafla fupi ya mahafali ya kidato cha nne ya Shule ya Sekondari ya Kilimanjaro Islamic iliyoko jijini Arusha.

Katika mahafali hayo, wanafunzi 73 walihitimu elimu ya kidato cha nne.

Alisema wanafunzi wengi wanapohitimu elimu ngazi ya vyuo na sekondari wamekuwa wakiishia kukaa mitaani na kujiunga kwenye makundi yasiyofaa na mwisho wake wanaharibika na kupoteza malengo yao.

Shahari alisema umefika wakati kwa shule za msingi na sekondari nchini, kuandaa mitaala na mfumo wa elimu ambao utawaandaa wanafunzi kutokuwa wategemezi pindi watakapohitimu mafunzo yao.

Sheikh Suleiman Mguluma aliwataka wazazi na walezi kuendelea kuwalea wanafunzi katika malezi na tabia njema, pindi watakaporejea majumbani mwao.

Aidha aliwataka wahitimu hao, kujijengea tabia ya kujiendeleza zaidi kwa kusoma kozi fupi wakati wakisubiri matokeo badala ya kuishia kukaa mtaani na kujiingiza kwenye makundi yasiyofaa ambayo yatawaharibia malengo yao waliyojiwekea.

Mkuu wa Shule ya Kilimanjaro Islamic, Kassim Mwasha, alisema shule hiyo tangu kuanzishwa imeongeza wenye ufaulu kwa mitihani ngazi ya taifa, mkoa na wilaya kila mwaka.

Meneja wa Shule hiyo, Sudi Kweka, alisema wamepanua wigo wa elimu shuleni hapo na kujenga shule ya wavulana na masomo yataanza rasmi mwakani.

Kweka alisema lengo la kuanzishwa kwa shule hiyo ya wavulana ni kuwawezesha kupata huduma kwa karibu zaidi kwa kuwa shule hiyo awali ilikuwa ya wasichana.

Aidha, Sudi aliwataka wahitimu hao kutanguliza uzalendo wa nchi huku akiwataka kujiendeleza zaidi na wasibweteke na elimu waliyoipata.

# Wafugaji watakiwa kusomesha watoto

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WASICHANA wa jamii ya kifugaji wametakiwa kusoma kwa bidii hadi kufikia malengo yao ya kimaisha badala ya kukimbilia kuozeshwa kimila wakiwa na umri mdogo hali ambayo itawagharimu kufikia ndoto zao.

Meneja wa Benki ya NMB, Tawi la Ngaramtoni, Lembris Lession, alisema wakati akizungumza na wazazi na wanafunzi katika mahafali ya 13 ya Shule ya Sekondari Mwandeti.

Katika mahafali hayo ambayo wanafunzi 320 wanahitimu kidato cha nne, alisema nyakati hizi wanafunzi wanatakiwa kusoma kwa bidii hadi kutimiza ndoto walizojiwekea na kuziweka kando mila potofu za kuozeshwa wakiwa na umri mdogo.

Alisema umefika wakati sasa wa watoto kutambua umuhimu wa elimu na kila mmoja anafikia malengo aliyojiwekea, hatimaye kupata kazi nzuri pindi atakapohitimu elimu ya juu.

Meneja huyo aliwataka wanafunzi hao kuchukua tahadhari dhidi ya makundi yasiyofaa watakapokuwa mtaani na waishi maisha waliyolelewa na walimu wao wakiwa shuleni sambamba na kutanguliza nidhamu.

Naye Mkuu wa shule hiyo, John Massawe, alisema pamoja na mafanikio makubwa kwa wanafunzi hao, bado wanakabiliwa na upungufu wa nyumba za walimu na nyumba zilizopo ni tisa.

Alisema matatizo hayo yamesababisha mahudhurio ya walimu kwenye vipindi kuwa hafifu kwa kuwa walimu wengine wanatembea umbali mrefu hadi kufika shuleni hapo na wakati wa mvua wanashindwa kuingia darasani kufundisha kwa kuhofia kunyeshewa na mvua barabarani.

Mkuu huyo wa shule alilitaja tatizo lingine kuwa ni ukosefu wa jengo la utawala katika shule pamoja na uzio.

Akisoma risala kwa niaba ya wahitimu wengine, Japhet Simon alisema pamoja na matatizo yaliyopo shuleni hapo, shule hiyo imekuwa ikifanya vizuri katika mitihani.

Simon aliishukuru serikali kwa kuleta mpango wa elimu bure ambao alisema umewasaidia wazazi wengi kuwa na mwamko wa kupeleka watoto shuleni.

# Takukuru yatolea ufafanuzi rushwa uchaguzi wa mitaa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Kilimanjaro, imeeleza kuwa hadi kufikia sasa haijapokea malalamiko yoyote yanayohusiana na rushwa katika uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika baadhi ya maeneo Jumapili iliyopita, Novemba 24.

Mkuu wa taasisi hiyo, Hole Makungu, aliyasema haya jana ofisini kwake wakati alipohojiwa na wanahabari kuhusu namna ambavyo uchaguzi ulivyofanyika.

Alisema kuwa uchaguzi huo ulifanyika vyema katika maeneo yote licha ya ushindani ulioji-tokeza katika Kijiji cha Kiraracha ambapo michuano hiyo ilikuwa kwa chama Mapinduzi CCM na Labour Part TLP. Kwa mujibu wa Makungu taarifa za matukio ya vitendo vya rushwa hazikujitokeza kutokana na vyama vingi vya upinzani kujitoa katika uchaguzi huo na kubakiza vyama vichache kwenye uchaguzi huo wa serikali za mitaa na vijiji. "Uchaguzi umemalizika salama na hakuna taarifa zozote zile za matukio ya rushwa na hii ni dalili njema kuwa watu wameshajua madhara ya rushwa kama ambavyo tumekuwa tukitoa elimu mara kwa mara,"alisema Makungu.

Taarifa hizo zimekuja ikiwa ni siku chache baada ya taasisi nne za kitaifa na kimataifa kutoa ripoti za kupungua kwa kiwango cha rushwa nchini kwa siku za karibuni tofauti na kipindi cha nyuma.

Makungu alizitaja taasisi hizo kuwa ni Twaweza, MO Ibrahim, Afro Barometer na Transparency International ambazo zimeonyesha kupungua kwa kiwango cha rushwa nchini sambamba na kukua kwa utawala bora kwa kiwango kikubwa.

Makungu alisema kuwa uchaguzi ni fursa au mchakato ambao watu wa eneo la uchaguzi wanaitumia kutafakari mustakabali wa maendeleo yao hivyo vitendo vya rushwa visingeweza kufumbiwa macho kwa kuharibu dhana nzima ya uchaguzi.



Mwakilishi wa Mkuu wa Chuo Kikuu Cha Kikatoliki Mwenge (MWECAU), Mhashamu Baba Askofu Severine Niwemugizi, akimtunuku Shahada ya Uzamivu Estomih Makyara, katika Mahafali ya 12 ya Chuo hicho, Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, mapema wiki hii.
**PICHA: DIXON BUSAGAGA**

# Utitiri wa madalali washtua wachimbaji

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WACHIMBAJI wa visima katika mikoa ya kanda ya kaskazini wameiomba Ofisi ya Bodi ya Maji Bonde la Pangani kuzifanyia uhakiki mashine mbalimbali zinazochimba visima katika mikoa hiyo kwa madai kuwa kumeibuka wimbi la kampuni za madalali zisizokuwa na vibali.

Wakizungumza jana katika kikao cha pamoja na viongozi wa wachimbaji hao, walisema kampuni hizo za madalali zimekuwa zikifanya kazi bila kuwa na vibali jambo linalowarudisha wananchi nyuma kimaendeleo.

Walilalamika kuwa wanakabiliwa na changamoto kubwa ya uwepo wa ongezeko la madalali wasio na vibali, licha ya wao kulipa tozo mbalimbali katika bonde hilo sanjari na kodi ya serikali inayolipwa kwenye Mamlaka ya Mapato (TRA).

Walisema wapo baadhi ya watumishi wasio waaminifu ambao hushirikiana na baadhi ya madalali wenye mashine zisizo na leseni jambo ambalo limekuwa ni changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

Walilalamika kuwa wapo baadhi ya watendaji ambao hushirikiana na madalali wasio na leseni wala mashine zao hazina leseni , jambo ambalo linawavuruga. Kukiwepo na ukaguzi wanajulishwa mapema na kuficha mashine wanazofanyia kazi. Hii inakatisha tamaa wachimba visima waliosajiliwa ambao wanaendelea kulipa kodi, wakati hawapati kazi nyingi za kuchimba visima kwani zimechukuliwa na wajanja hao.

Mkuu wa Idara ya Maji ya Ardhini wa Bonde la Pangani, Amiri Msangi alisema wamepokea changamoto za wachimbaji na watazifanyia kazi ili kudhibiti uwepo wa madalali .

Alisema sheria inaelekeza mchimbaji awe na kampuni ndipo apewe leseni ya uchimbaji pamoja na uwepo wa ukaguzi wa mara kwa mara wakati wa uchimbaji ili kuleta matokeo chanya kwa mteja na kutoleta madhara kwa wateja.

Akijibu changamoto Ofisa wa Bodi ya Maji Bonde la Pangani Segule Segule, alisema wamepokea changamoto hizo za ongezeko la madalali lakini zitafanyiwa kazi katika kuongeza tija na mabdailiko lengo likiwa kila mmoja aweze kufuata sheria na taratibu zilizowekwa.

"Tutatoa namba zetu za simu ikiwa mtaona ukiukwaji wa sheria hizi, toeni tarifa na hatua kali za kisheria zitachukuliwa ili kutokomeza ukiukwaji wa sheria na taratibu ,"alisema Segule.

# Wataka ulinzi skimu ya umwagiliaji

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAKULIMA wa mboga na matunda katika skimu ya umwagiliaji ya Lower Moshi, wameiomba serikali kuongeza ulinzi katika usimamizi wa miundombinu hiyo ili kuleta tija kwa Watanzania.

Hayo yalisemwa jana wakati wa ziara ya timu ya wataalam kutoka Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Mkoa wa Kilimanjaro kwa ajili ya ukaguzi wa miundombinu ya umwagiliaji.

Mmoja wa wakulima hao, Severin Msofe, alisema ni vyema tume kwa kushirikiana na serikali kuanzisha utaratibu maalumu wa kusimamia miundombinu lengo likiwa kutoharibiwa na baadhi ya watu wasio waaminifu.

"Tunaomba kutungwe sheria ambayo itawabana wenyeviti wa vijiji, vitongoji na wasimamizi wa skimu hizi kulinda na kutunza miundombinu katika skimu hizi. Wako baadhi ya watu wasio waaminifu huharibu miundombinu hiyo bila kujali gharama zinazotumika na serikali kutengeneza," alisema.

Alisema Sheria ya Umwagiliaji Na. 5 ya mwaka 2013, inamtaka kila mkulima kulinda miundombinu na atakayekiuka, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Skimu ya Lower Moshi iko umbali wa kilomita tano kutoka Moshi Mjini na ilijengwa mwaka 1984 kwa gharama ya Sh. bilioni tatu kwa ufadhili kati ya serikali ya Tanzania na Japan kupitia Shirika la Maendeleo la Japan (JICA).

Aidha, skimu hiyo ni miongoni mwa miundombinu bora ya umwagiliaji nchini ambayo wakulima wake wanalima mpunga kwa wingi na kufuata mwongozo kabambe wa umwagiliaji.

Eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji ni zaidi ya hekta 2,000 lakini eneo lililoendelezwa kwa miundombinu bora ya umwagiliaji ni hekta 1,100, sawa na asilimia 55.

Vyanzo vya maji katika skimu hii ni mto na chemchem za Njoro na Mandaka ambazo hupeleka maji kwenye mabanio ya Mabogini na Rau.







Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, akizungumza na wenyeviti na wajumbe wapya wa serikali za mitaa, waliochaguliwa kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), baada ya kuapishwa, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Msako wanaokata nyama kwa magogo watangazwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BODI ya Nyama nchini inatarajia kuanza msako wiki ijayo kwa wafanyabiashara wa mabucha ya nyama na samaki wanaotumia magogo kukata nyama.

Imesema msako huo pia utaangazia kundi la wafanyabiashara wanaobeba nyama begani, ikiwaagiza kuzingatia kanuni za usafi katika sehemu za biashara zao ili kujiepuka na magonjwa ya mlipuko.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, Kaimu Msajili wa bodi hiyo, Imani Sichalwe, alisema msako huo utajumuisha timu ya bodi na watalaamu wa afya ili kuwachukulia hatua wafanyabiashara wasiozingatia masharti yaliyowekwa kwa wauzaji wa nyama.

"Mfano, suala la ubebaji nyama mgongoni ni hatari kwa afya ya jamii kwa sababu nyama inapogusa migongo ya watu, inasababisha jamii kupata magonjwa yatokanayo na uchafu," alisema. "Hata makoti wanayovaa wabebaji, baadhi si safi na hivyo kuhatarisha afya za walaji. Hakuna kubeba nyama mgongoni wala kichwani, unapoishusha katika gari la nyama mnapaswa kushikishana mikononi na siyo kujitwisha," alisema.

"Kukatia nyama kwenye magogo ni hatari sana, vijiti huchanganyikana na nyama, jambo ambalo ni hatari kwa afya ya binadamu."

Ofisa Usajili wa bodi hiyo, Godfrey Sosthenes, alisema wauza nyama wote wanapaswa kujisajili ili iwe rahisi kuwatambua katika maeneo wanayofanyia kazi.

"Kuanzia wiki ijayo, tutasajili wafanyabiashara wa mabucha ili kuwatambua idadi yao na kuwaelekeza masharti ya ufanyaji biashara hiyo," alisema.

# FCC yashauriwa kutoa elimu shule za vijijini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Ushindani (FCC) imeombwa kutoa elimu ya kutambua bidhaa katika shule za vijijini kwa kuwa maeneo hayo yanakabiliwa na tatizo la uuzwaji wa bidhaa zilizovuka muda wa matumizi.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mlezi, Anicetus Lyimo, wakati wa mkutano wa kutoa elimu kwa mtumiaji wa bidhaa zilizomaliza muda ulioandaliwa na tume hiyo jijini hapa.

Alisema jamii inayoishi vijijini, inahitaji elimu hiyo kwa kuwa wengi wamekuwa wakitumia bidhaa zilizopitwa na wakati.

"Hii elimu inapaswa kutolewa vijijini kwa sababu asilimia kubwa ya watu hawana uelewa juu ya ulaji," alisema.

Awali, Ofisa Mwandamizi wa Mawasiliano na Uhusiano wa Umma wa FCC, Frank Mdimi, alisema tume imeanzisha klabu tano za wanafunzi wa shule za msingi jijini Dodoma ambazo zitatoa elimu kwa wanafunzi na jamii kuhusu matatizo ya ununuzi na matumizi ya bidhaa zisizo na ubora.

Mdimi alisema kuanzishwa kwa klabu kwenye shule nchini ni sehemu ya mikakati yao kufikisha elimu kwa watumiaji wa bidhaa.

Alitaja shule ambazo klabu hizo zipo kuwa ni Shule ya Msingi Mlezi, Chadulu, Mlimwa B, Martin Luther na Kikuyu.

"Lengo ni kudhibiti bidhaa bandia, namna gani wanafunzi wanaweza kuwasilisha malalamiko pamoja na kufundisha haki na wajibu wa mlaji katika kukabiliana na matatizo ya ununuzi na matumizi ya bidhaa zisizo na ubora zilizoko sokoni," alisema.

Mdimi alisema malengo yao ni kuanzisha mitaala ili kujenga jamii yenye uelewa kuanzia ngazi ya chini ya familia mpaka ngazi ya juu kielimu.

Mwanafunzi wa Shule ya Msingi Mlezi, Salma Ally, alisema elimu hiyo imemsaidia kuepuka madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa zilizovuka muda wa matumizi kwa kuwa sasa kabla ya kununua bidhaa, anaangalia muda wa kuisha kutumika.

# Serikali yaamua kutotumia makandarasi miradi ya maji

**Na Augusta Njoji,** MPWAPWA

SERIKALI imeamua kutumia wataalamu wake kutoka Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa) kutekeleza miradi ya maji nchini kutokana na makandarasi kutofanya kazi kwa uaminifu.

Imesema kukosekana kwa uaminifu kumesababisha miradi mingi ya maji kukwama kwa muda mrefu huku mingine ikitekelezwa chini ya kiwango, hivyo serikali kupata hasara.

Akizungumza jana wilayani Mpwapwa akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maji, Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, alisema wameshaanza kuufanyia kazi uamuzi wao huo katika maeneo yenye matatizo makubwa ya upatikanaji wa maji, akiitolea mfano mikoa ya Rukwa na Kigoma.

Alisema makandarasi wengi wamekuwa wajanja na wamekosa uaminifu, hali iliyosababisha serikali kuamua kujipanga upya kwa kujenga yenyewe ili kuhakikisha huduma ya maji inafika kwa wananchi.

"Najua hii ni vita, lakini tumeamua tunachukua wataalamu wetu wa Ruwasa, tunawapa miradi, tunawapa hela, wanatekeleza miradi.

"Tukiendelea na utaratibu wa kuwapa wakandarasi, hatutatoka kwa sababu mkandarasi akichukua mradi ameshamwahidi huyu kumpa asilimia 10, na yeye anabaki na pesa kidogo, miradi inakwama," Prof. Mbarawa alisema.

Aliongeza kuwa kwa miezi mitano sasa, hawajatoa kibali cha ujenzi kwa wakandarasi kutokana na ujanja ujanja walioubaini.

"Ukisikia mradi ni Sh. bilioni 1.170, ujue siyo gharama yake halisi, hapo gharama yake ni Sh. milioni 600.8, au 900, ukimuuliza anakwambia 'ilikuwa nigawe huku nigawe huku', sasa mkandarasi hutakiwi ufikirie hayo, unatakiwa ulete thamani ya mradi unaotakiwa kutekeleza.

"Hiyo ndiyo changamoto iliyokuwapo lakini tumeamua kujipanga sasa kupambana kuhakikisha miradi tuliyopanga kutekeleza inamalizika, lakini miradi mipya kwa asilimia kubwa hatutawapa makandarasi tena, tutawapa makandarasi kazi ambazo sisi hatuna uwezo nazo.

"Naamini kama wataalamu wetu hawana uwezo, sifikirii kama wakandarasi watakuwa na uwezo nazo," alisema. Alisema kwa muda mrefu miradi ya maji ndiyo imekuwa mahala pa kila mtu kula fedha, akisisitiza ulaji huo sasa hauna nafasi tena.

"Hapa kuna mradi ulikuwa unalipiwa na World Bank (Benki ya Dunia) wa miaka 10, lakini maji hayatoki kwa sababu mimi, wewe na wote tumeshiriki kukwamisha, makandarasi walipewa wasio na uwezo na haikuwa kwa bahati mbaya.

"Wengine viongozi walitengeneza kampuni zao zisizo na uwezo, mradi miaka 11 haukamiliki, hapa utamnyooshea mtu kidole, lakini lazima tuseme ukweli, kwa sasa hatutaki kuangalia nyuma, tunataka wananchi wapate maji," alisema.

Awali, akisoma taarifa ya hali ya upatikanaji wa maji, Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri, alisema Mkoa wa Dodoma una miradi inayotekelezwa lakini kwa kiasi kikubwa inakabiliwa na vikwazo kukamilisha.

"Mpwapwa tuna miradi 10 inayotekelezwa na mfuko wa maji, miradi saba ni mipya na mitatu ni ya ukarabati yenye thamani ya Sh. bilioni 4.17.

"Katika miradi hii, kazi kubwa zimefanyika ikiwamo kujenga matenki ya kuhifadhi maji, lakini hatua ya ukamilishaji inakwama katika miradi mingi kutokana na changomoto ya pampu na kuunganisha umeme," alisema.

Alisema upatikanaji wa maji imeongezeka kutoka asilimia 43 mwaka 2015 hadi asilimia 57 mwaka huu. "Katika miji midogo na wilaya ni asilimia 68, Jiji la Dodoma asilimia 82, lengo ni kuongeza upatikanaji wa maji kufikia asilimia 90 kwa miji midogo na wilaya na Jiji la Dodoma kufikia asilimia 95 ifikapo 2020," alisema.

Alibainisha kuwa upande wa vijijini, hali ya upatikanaji wa maji kwa mkoa ni asilimia 57, lengo likiwa ni kufikisha asilimia 85 mwakani.







Rais wa Mahakama ya Afrika, Slyvain Ore (katikati) kutoka nchini Cote d' Ivoire, akiongoza kikao cha 55 cha Mahakama hiyo, kilichofanyika kwa mara ya kwanza mjini Zanzibar juzi. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Waanzisha mpango wa amani Zanzibar

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

KATIKA kuelekea mwaka 2020 ambao ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu Tanzania, Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Ofisi ya Mufti, imezindua mradi wa uhamasishaji uitwao 'Seaching for a Common Ground for Peace in Zanzibar' ili amani iwapo wakati wote kabla na baada ya uchaguzi.

Lengo kuu la mradi huo ni kuongeza maelewano na ushirikiano wa kidini na kiutamaduni kwa jamii kwa kuanzisha mazungumzo ya pamoja kwa ujenzi wa amani ya Zanzibar.

Akizungumza katika uzinduzi wa mradi huo, Mshauri wa Waziri wa Katiba na Sheria katika masuala ya dini, Sheikh Fadhil Suleiman Soraga, alisema jana kuwa viongozi wa dini ndio walezi wa amani katika jamii yoyote.

Soraga alisema kulikuwa na wakati Tanzania ilikuwa katika majaribu na baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa waliandaa mkakati wa kufanya matembezi (mkakati wa ukuta) na nchi ilikuwa katika taharuki kubwa.

Alisema matembezi hayo yangeleta athari kubwa na amani ingeharibika lakini viongozi wa dini walifanya jitihada ya kukutana na viongozi hao na kutumia hekima ili waache mpango huo. Viongozi hao waliheshimu mawazo ya viongozi wa dini na maandamano hayo hayakufanyika.

"Ulipofutwa uchaguzi wa Zanzibar mwaka 2015, viongozi wa dini tulikutana na viongozi wa vyama vya siasa ili nchi iwe katika hali ya utulivu. Tuliongea na Maalim Seif (Sharif Hamad) ambae alikuwa mgombea wa urais kupitia CUF na kwa kweli tulimpongeza kwa usikivu na alituahidi kuwa atatuliza wanachama wake na nchi haitaharibika kwa sababu ya yeye na amani ilitawala," alisema.

Sheikh Soraga alisema wakati wa uchaguzi nchi huwa katika misukosuko mikubwa kwa hivyo mradi huo umekuja muda muafaka na amani ni muhimu na ndiyo kila kitu.

Naye Mufti wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kabi, alisema Zanzibar ilipita katika misukosuko mikubwa ikiwamo makanisha kuchomwa moto, misikiti kupigwa mabomu kutokana na wananchi kutokuwa na imani ya kiroho.

Aliwataka viongozi wa dini kuwaelewesha wananchi kiroho kuwa dini zote zinapigania imani na amani, hivyo tofauti za vyama isiwe sababu ya kubaguana, kuoneana na kufanya vitendo vya uvunjifu wa amani.

"Amani inakuja kwa wale wenye imani na ikiwa hawajafanya vitendo vya dhuluma. Kwa hivyo sisi viongozi wa dini tujitahidi kuwafahamisha watu wetu kila mmoja kumjali na kumheshimu mwezake.

Ikiwa tutafanya hayo, naamini kuwa mwaka 2020 mwanzo hadi mwisho itakuwa amani tupu na kwa mwaka huo tujitahidi sana tuwe tofauti na miaka iliyopita ya uchaguzi" alisema.

Naye Katibu Mkuu wa Kanisa la Anglikana, Canon Stanley Lichinga, aliwataka viongozi wa vyama siasa kuyatumia majukwaa yao kuhamasisha amani.

Alisema si vyema damu ikamwagika au wananchi wakauwawa kwa sababu ya kutafuta viongozi wao au kwenda katika mikusanyiko ya kupiga kura katika uchaguzi mkuu.

# SMZ yasaka mzabuni kusambaza mchanga

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema iko katika mchakato wa kutafuta wakala wa kuuza mchanga kwa lengo la kuwawezesha wananchi wa kawaida kupata huduma hiyo kwa bei rahisi.

Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Dk. Makame Ali Ussi, alisema jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Magomeni, Rashid Makame Shamsi, aliyetaka kujua utaratibu wa wananchi wa kawaida kupata huduma ya mchanga imefikia wapi hadi sasa.

Alikiri kwamba upatikanaji wa mchanga kwa wananchi wa kawaida umekuwa na changamoto mbalimbali kiasi cha wengi kushindwa kumudu kupata.

Ussi alisema awali wizara ilitayarisha mfumo ambao ni rafiki kwa ajili ya kuwawezesha wananchi wa kawaida kupata mchanga bila ya usumbufu.

"Mheshimiwa Spika Wizara iko katika mchakato ambao utawawezesha wananchi wa kawaida kupata huduma ya rasilimali ya mchanga bila ya usumbufu," alisema.

Naibu waziri huyo alisema wizara inachukua kila aina ya tahadhari katika suala la mchanga na kuona kwamba rasilimali hiyo inatumika vizuri kwa faida ya wananchi wote.

Alisema hali ya mchanga Zanzibar si nzuri na kwamba umakini wa matumizi yake unahitajika ili kuwawezesha wananchi wengi kufaidika na rasilimali hiyo.

Alisema hivi sasa baadhi ya miradi ya ujenzi ya serikali imechelewa kumalizika kwa wakati kwa sababu ya ukosefu wa mchanga.

# Makamishina utawala bora wapewa somo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Tume ya Maadili Zanzibar, Asaa Ahmad Rashid, amewataka makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kufanya kazi kwa uadilifu ili wananchi wanufaika na haki zao.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, katika ufunguzi wa mafunzo ya siku tatu kwa makamishna wa haki za binadamu Bweni nje kidogo ya Mji wa Zanzibar, alisema wananchi bado wamekuwa wakikosa haki za msingi katika jamii kutokana na baadhi ya watendaji kutokuwa waadilifu katika kutekeleza majukumu yao.

Rashid alisema wananchi wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo udhalilishaji katika jamii na sehemu za kazi jambo ambalo limekuwa likichangia uvunjifu wa haki za binadamu nchini.

Alisema ili kuimarisha misingi ya upatikanaji wa haki za binadamu, ni vyema kwa makamishna kuona umuhimu wa kufuata sheria za kazi ikiwamo kuwa waadilifu, kuondoa urasimu na rushwa ili kuimarisha upatikaji wa haki za binadamu kaika jamii.

Pia alisema tume itakaposimamia vyema, upatikanaji wa haki za binadamu kwa rika zote itaongeza kasi ya upatikaji wa amani katika nchi.

Mwenyekiti huyo aliwataka watendaji wa tume hiyo kuandaa mpango maalumu wa utoaji wa elimu kwa wananchi juu ya kujua haki zao ili kuimarisha upatikanaji wa huduma muhimu pamoja na kuwawezesha kuripoti kesi za ukiukwaji wa haki za binaamu katika vyombo husika.

Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Fatma Muya, alisema watahakikisha wanafanya kazi kwa mujibu wa sheria ili wananchi wanufaika na haki zao kwa wakati.

Alisema tume imekusudia kufanya utafiti juu ya masuala ya udhalilishaji kwa wanawake na watoto ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakikosa haki zao katika sekta za umma na familia wanazoishi.

Alisema kundi kubwa linalokosa haki zao katika jamii ni wanawake na watoto jambo ambalo linarejesha nyuma juhudi zao katika harakati zao za kiuchumi, kijamii na kimaendeleo.

Mmoja wa makamishna walioshiriki mafunzo hayo, Khatib Mwinchande, alisema watahakikisha wanayafanyia kazi mafunzo walioyapata ili kuongeza upatikaji wa haki na utawala bora.

Alisema kila mwanchi ana haki ya kupata haki zake pamoja na kuepuka uvunjifu wa haki za binadamu kwa lengo la kuunga mkono juhudi za serikali katika kuimarisha huduma za maendeleo zinazotokana na uadilifu wa utawala bora.



## BI CHEKA

Soma UK.14

JUMAMOSI NOVEMBA 30, 2019



# WEMA VS IDRIS

## VITA INAYOUNGURUMA TARATIBU

Soma UK.14

## BASI SAWA



## Wengi wamlilia Bi Cheka

WASANII mbalimbali wameonesha simanzi zao kufuatia kifo cha mwanamuziki wa Bongo Fleva, Cheka Hija maarufu kama Bi Cheka ambaye aliaga dunia juzi mchana.

Bi Cheka aliaga dunia wakati akipatiwa matibabu katika Hospital ya Rufaa ya Mloganzila baada ya kusumbuliwa na matatizo ya moto.

" Mara ya mwisho nakumbuka alikuwa akisumbuliwa na Moyo na Presha, toka tupo naye kimuziki alishaanguka kwenye stage mara mbili na hata sisi wenyewe tulipewa ushauri na kiongozi mmoja mkubwa na daktari wakisema huyu anatakiwa kupumzika, Mungu amueweke mhali pema peponi," Mh. Temba



## Wasanii wamsusa mama wa Sharo Milionea

MAMA mzazi wa marehemu Sharo Milionea, amesema anasikitika kuona baadhi ya wasanii waliokuwa karibu na mwanawe wameanza kumsusa.

Amesema kila mwaka wamekuwa na kawaida ya kufanya dua ya kumbukumbu ya siku ya kifo cha mwanae kilichotokea November 26, lakini kwa miaka mitatu hakuweza kusoma kutokana na wasanii hao kuingia mitini.

"Kila mwaka nilikuwa nasaidiwa kusoma dua ya mwanangu, lakini nilishindwa kwa miaka mitatu baada ya wasanii kunikimbia lakini mwaka huu namshukuru Irene Uwoya na wenzake kunikumbuka," amesema.



# WEMA VS IDRIS VITA INAYOUNGURUMA TARATIBU

WIKI ya mpambano kati ya timu za mastaa wawili nchini, Idris Sultan na Wema Sepetu, kwenye mitandao ya kijamii ni kuchambana na kutoleana maneno makali kwenda mbele.

Vita hiyo ambayo ilionekana kama mzaha, lakini kila muda unaposonga mbele moto unazidi kuwaka kiasi ambacho kinahatarisha wasanii hao ambao huko nyuma walikuwa wapenzi.

Chanzo cha kuibuka malumbano hayo makali kwenye mitandao ya kijamii ni kutokana na ujumbe uliowekwa kwenye akaunti ya Insta ya Idris ambao umetafsiriwa ni kijembe kwa Wema.

Baada ya kuweka ujumbe huo, timu ya Wema ilianza kuja juu wakimshambulia Idris kwa maneno makali ambayo timu ya mchekeshaji huyo haikuvumilia nao wakajibu mapigo kwa kumtetea.

Idris aliandika hivi: "Najua ni asubuhi ila nikiona selebriti mwingine aliyekonda kwa stress au kukosa hela ya kula halafu anakuja kututangazia dawa za kupunguza unene wakati hata hazijui wala hazitumii, hazifanyi kazi, najitolea kumnyonga."

Wewe msomaji unakuwa upande upi kutokana na ujumbe huu wa Idris?

## INSTA-TWITTER





**Rafiki** yangu naomba nikuambie. Passo yako ya kuuza mayai ya kanga ni tamu na ya amani kuliko benzi la kuhongwa- **Idriss Sultan.**



**Kama** uko na mpenzi ambaye ana tabia ya kutokupokea simu zako au kutojibu text zako za asubuhi anakujibu kesho, ama unampigia saa moja asubuhi hapokei anakuja kukupigia baada ya masaa kumi, basi na wewe usimpigie simu wala kumtext kwa siku kumi! Kwa sababu ameamua kukuchezea michezo ya kitoto, basi mpe siku kumi za kuwa mkubwa- **Mwijaku**.



## Nuh Mziwanda kawa kama kinyonga

MWANAMUZIKI nyota, Nuh Mziwanda, amesema kubadilika kimuziki kila wakati kunamfanya kuwa na ushawishi wa kipekee kwa mashabiki wake.

Akizungumza hivi karibuni, Nuh amesema wimbo wake mpya 'Amina' ni alama tosha kwamba yeye ni mtu wa kubadilika kutokana na kufanya utafiti nini wafuasi wake wanataka.

"Kawaida yangu napenda kubadilika kutokana na wakati, nashukuru Mungu mashabiki wangu wananikubali na kila nikitoa ngoma wanaipokea vizuri kutokana na kukata kiu zao," amesema Mziwanda.






**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

**@burudanitele**

# ESHA ATAFUTA UGOMVI KWA MLELA, HEMED

MWIGIZAJI wa Bongo Muvi, Esha Buheti, amepasua jipu baada ya kusema hadharani kwamba wasanii wa kiume Yusuph Mlela na rafiki yake Hemed Suleiman (PHD) wanapenda kulelewa.

Buheti ametoa kauli hiyo wakati akizungumza kwenye kipindi cha Kikaangoni kwenye kurasa za Facebook na YouTube ya EA TV na kueleza ana habari kwamba wawili hao wanahudumiwa na wanawake zao.

"Ni kweli unajua kuna wasanii ambao mimi nawafahamu japo wengine unajua siwezi kuwataja kwa sababu najua nitagombana nao bure.Ila kwa sasa ninaowafahamu ni Mlela na rafikiyake Hemed PHD'; amesema Esha.

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Mara** paap, ma ex wako wote wanakutumia Sh. 10,000. Hivi utakuwa na Shilingi ngapi?-**Mkude Simba**



**Usidharau** nafasi yoyote ambayo unayo kwa sasa, maana kuna wengine wanatamani kufika ulipofika wewe-**Nandy.**



**Mkono** shavuni nawaza siku inavyokwenda, maadui wamenizunguka, sina rafiki.
Wengi ni mashabiki pembeni wananicheka, nimeshushwa thamani kama shillingi moja-**Timbulo.**

# Kuumbe!



# TABORA KUMEKUCHA

## ALI KIBA ATETEMESHA NA 'UNFORGETABLE'

MFALME wa muziki wa Bongo Fleva, Ali Salehe Kiba maarufu kwa jina la Ali Kiba, ameonesha umwamba wake baada ya kuitetemesha vilivyo Mkoa wa Tabora katika mwanzo wa ziara yake ya kimuziki.

Tangu atue mkoani humo, umati wa watu umekuwa ukimfuatilia kuanzia mapokezi yake hadi alipokuwa akifanya zake za kijamii anazofanya katika mji wa Tabora.

Alikiba yupo mkoani humo kwa ajili ya tamasha lake la 'Uniforgetable' linalofanyika leo katika uwanja wa Ali Hassan Mwinyi. Awali alipanga kuzindua mkoani Mwanza, lakini kutokana na sababu mbalimbali ameamua kuhamishia Tabora.

Alipotua mkoani humo akitokea Dar es Salaam, umati wa watu ulimpokea kwa shangwe huku wakimsindikiza kwa maandamano ya baiskeli, pikipiki na magari hadi sehumu aliyofikia.

Mapokezi ya kipekee aliyopewa Ali Kiba ni dalili tosha kwamba bado anapendwa na jina lake linazidi kutikisa katika masikio ya mashabiki wa muziki.

Kiu ya Wanatabora ni kuona mwanamuziki huyo anawatendea haki kwa kutoa burudani itakayokonga nyoyo zao na kuthibitisha kwamba hakuna Mfalme wa muziki kuliko yeye.

Ahadi aliyotoa kwamba tamasha hilo litakuwa la kipekee nchini ni matarajio ya wengi kuwa itatimizwa kwa kupiga muziki unaoeleweka na jukwaa kupambwa na wasanii wenye vipaji.

Imani ya mashabiki wengi ni kuona 'Uniforgetable' ni tamasha ambalo halitasahaulika kama jina lenyewe lilivyo, hasa kwa Ali Kiba kutumia ujuzi wake wa kutoa zaidi ya burudani na si mikogo na uwezo wa kifedha kama wanavyofanya wasanii wengine.

# Wapuliza tarumbeta wanavyodatisha vigodoro



**Roman Mng'ande kulia na Hamisi Mnyupe kushoto**

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE miaka ya karibuni imekuwa si rahisi kuona muziki wa dansi umehanikizwa na chombo cha muziki kiitwacho 'trumpet' kwa kiswahili tarumbeta.

Bendi karibia zote za muziki wa dansi za zamani kuanzia miaka ya '50 hadi mwishoni mwa '90 zilikuwa ni lazima ziwe na ala za upepo ikiwamo tarumbeta, tena zikipigwa na watu kuanzia watatu hadi watano wakati mwingine.

Mwanzoni mwa mwaka 2000, yalipokuja mapinduzi na muziki kwa ujio wa bendi za African Stars 'Twanga Pepeta', Diamond Sound, FM Academia na nyinginezo, ziliacha kutumia ala za upepo kama tarumbeta, saxaphone na vingine vinavyofanana na hivyo na badala yake kutumia zaidi kinanda.

Bendi kuu nchini Tanzania Msondo Ngoma Music Band, DDC Mlimani Park Orchestra, Vijana Jazz na zile za majeshi, bado zinaendelea kutumia ala ya trumpet, lakini si wasanii wa muziki wa bongo fleva au bendi za muziki zilizobaki zinazotumia ala hiyo.

Kwa sasa utamu wa chombo hicho umebakia kwenye muziki wa vigodoro ambapo ala za upepo ikiwemo tarumbeta hupigwa huko na kuwapagawisha akinamama vilivyo kwenye masherehe mbalimbali za kijamii.

Wafuatao ni baadhi ya wapiga trumpet hodari kwenye muziki wa dansi Tanzania.

**Roman Mng'ande 'Romario'**

Huyu ndiye mpiga trumpet maarufu sana kwenye kizazi cha sasa. Na amekuwa maarufu zaidi si kwa sababu ya kupiga trumpet tu, bali hasa machachari yake kwenye kurap, na kucheza hasa akiwa tumbo wazi, huku akikatika.

Ni mwanamuziki wa muda mrefu kwenye kundi la Msondo Ngoma Music.

**Machaku Salum**

Alikuwa mpiga trumpet maarufu kwenye bendi ya Sikinde. Umaarufu wake alitokana na upigaji chombo hicho pamoja na utanashati wake anapokuwa jukwaani.

Machaku ambaye ameshafariki dunia, ndiye baba mzazi wa aliyekuwa mchezaji wa zamani wa Simba, Salum Machaku.

**Hamisi Mnyupe**

Ni mpiga trumpet mahiri nchini ambaye kwa sasa anapigia bendi ya Msondo Ngoma Music.

Hata hivyo, kabla ya bendi hiyo alishawahi kupitia kwenye bendi za Uda Jazz na Vijana Jazz na hadi leo analisongesha gurudumu la muziki wa dansi nchini akiwa anapiga chombo hicho.

**Joseph Lusungu**

Kiongozi, mtunzi, mpanga muziki, mwalimu na mpiga trumpet wa kiwango cha hali ya juu aliyewahi kuishi nchini.

Ana uwezo wa kuachiwa kipande na kupiga peke yake kwa dakika hata tano, akiwa na uwezo pia wa kupiga kwa staili ya macharanga na muziki wa Cuba na Amerika ya Kusini. Alikuwa ni mmoja wa viongozi wa bendi ya Msondo Ngoma hadi alipofariki.

**Mawazo Hunja Shaurimbele**

Kijana mmoja mtanashati, mwenye uwezo wa hali ya juu kwenye upigaji wa chombo hicho.

Hadi anafariki, alikuwa anapigia bendi ya Vijana Jazz, akiwa amechukuliwa kutoka Super Matimila.

# IMETOKEA

TUKIO hili limetokea mwaka 2014 pale mrembo Hayden Panettiere alipojikuta akianguka kwenye ngazi wakati akijiandaa kuongoza maonesho ya bidhaa mbalimbali ya kisanii.

Maonesha hayo yalifanyika katika ukumbi wa Metropolitan Museum of Art, na kusababisha waalikwa kutaharuki.

Panettiere alipendeza vilivyo kutokana na gauni lake refu la rangi nyeupe, lakini alipogusa zulia jekundu akishuka kwenye ngazi, ghafla alilikanyaga na kuanguka chini.







# CATHERINE Shemeji anapozima taa

**Na Adam Fungamwango**

UMDHANIAYE ndiye kumbe siye. Na umdhaniaye siye kumbe ndiye.

Unaweza kupata matatizo au mkasa ambao hujui chanzo chake ni nini.

Wakati mwingine anaweza kuwa ni ndugu wa damu ndiyo anakuumiza.

Filamu ya 'Catherine' inaweza kuwa mfano tosha wa haya ninayosema.

Filamu hii imechezwa na magwiji wa tasnia hiyo nchini kama Hemed Suleiman, Jackline Wolper na msanii anayekuja kwa kasi Najma Dattan, pamoja na msanii wa bongo fleva Hamad Ally 'Madee'.

Hemed anatokea kumpenda Najma ambaye ni dada wa Madee, huku wao wenyewe wakiwa na marafiki wa damu.

Hata hivyo, Madee anapinga rafiki yake Hemed kumpenda dada 'ake kwa madai kuwa hajatulia.

Hemed anamhakikisha Madee kuwa ni kweli amekuwa kicheche, lakini kwa Najma atatulia na hatimaye kumuoa kabisa na wala hana nia ya kumchezea, kitu ambacho kinapingwa vikali ya rafiki yake huyo.

Mapenzi ya Hemed na Najma anakuwa motomoto kiasi cha kwamba hakuna tena mtu wa kuyazuia kiasi cha kufikia posa kutolewa.

Kabla ya ndoa anawasili kutoka nchini Marekani alikokwenda kwa masomo dada wa Najma ambaye ni Wolper aliyecheza kama Sharon.

Aina yake ya maisha akawa anaijua mwenyewe, kwani ni tofauti na Najma ambaye amelelewa katika mazingira ya kumcha Mungu.

Sharon, binti aliyeishi kwenye nchi za watu, mwenye kuyajua ya usiku na ya mchana anaanza kuona wivu mdogo wake kuwa na mvulana 'handsome'.

Anatumia kila aina ya hila ili kumgombanisha Najma na Hemed na anafanikiwa.

Anamtumia kijana mmoja 'kumpaka' Najma mbele ya mchumba wake kuwa amekuwa akitembea na mume wa dada yake kiasi kwamba amesababisha dada yake kukosa amani kwenye ndoa.

Pia kijana huyo anatuma meseji za mapenzi kwenye simu ya Najma kwa kutumiwa na Sharon.

Hemed anachukia na kuachana na mchumba wake, lakini pia akiingia kwenye penzi la siri na dada wa mchumba wake Sharon. Shemeji shemeji kumbe wanazima taa.

Za mwizi arobaini, Najma anawafuma 'live' kitandani dada yake na mchumba 'ake kitu ambacho kinasababisha achanganyikiwe na kukimbia mbio kiasi cha kugongwa na gari.

Sharon naye baada ya kuona hila zake zimegundulika anaamua kunywa vidonge kwa ajili ya kujiua, lakini anapona.

Kikao kikubwa kinafanyika na kila kitu kinagundulika.

Filamu inaisha kwa Hemed kufunga ndoa na Najma.



# MDOMO UMEMPONZA

## T.I SASA APIGA MAGOTI AHURUMIWE

UKISIKIA mdomo umemponza kichwa ndiyo huku! Sasa rapa Clifford Harris Jr.,maarufu kama T.I, ameanza kujilaumu mwenyewe baada ya kutoa kauli tata kuhusu binti yake.

Hivi karibuni mwimbaji huyo alikaririwa akisema kwamba huwa na kawaida ya kumpima binti yake ili kujihakikishia kama bado anatunza bikra yake.

Baada ya kutoa kauli hiyo, watu mbalimbali walijitokeza kumshutumu kwa kitendo hicho na wengine walikwenda mbali kwa kumtaja kama si baba bora kwa binti yake.

Sasa TI ameamua kuunda jopo la kumtetea kutoka katika kitanzi alichokifunga mwenyewe.

Katika jopo ambalo linawajumuisha mkewe, Tameka “Tiny” Harris na Jada Pinkett Smith walikwenda kwenye kipindi cha “Red Table Talk” na kulitolea ufafanuzi suala lake.

Wote watatu walitetea kwa nguvu kuwa T.I anapompeleka binti yake Deyjah Harris kwa daktari wa wanawake kumuangalia kama bado ana usichana wake huwa haingii chumba cha daktari.

Katika kipindi hicho T.I alisema “Maana yangu ilitafsiriwa tofauti, acha niweke mambo sawa. Sikusema kwamba nilikuwa naingia naye kwenye chumba cha daktari. Hiyo ni kunitafsiri vibaya. Huo ni Uongo. Na pia sikusema wamba huwa ninafanya hilo kwa siku hizi,”

Akaongeza “Sasa hivi tayari ana umri wa miaka 18, siwezi tena. Sikusema wamba mama yake anakuwa hayupo, mama yake huwa anakuwapo na kila kitu.”

Katika kuonesha amejutia, rapa huyo alimuomba radhi binti yake Deyjah na pia aliweka wazi kuwa alikuwa anafanya vile wakati binti yake huyo akiwa na umri wa miaka 15 na 16.

Katika mahojiano kati ya T.I. katika kipindi cha “Ladies Like Us” kinachoongozwa na Nazanin Mandi pamoja na Nadia Mohan yaliyoibua sakata hili na kufutwa mtandaoni yalikuwa na athari kubwa katika familia yake.

Binti yake huyo aliamua kumfuta urafiki baba yake mzazi na kisha kufuta akaunti zake za mitandao ya kijamii kitendo kilichoibua hisia kali.

# French Montana apata nafuu



WIKI hii mashabiki wa muziki nchini Marekani walijaa hofu baada ya mwanamuziki French Montana kuripotiwa kuwa ni mgonjwa.

Iliripotiwa kuwa French kafikishwa katika hospitali kubwa nchini Marekani kupatiwa huduma ya matibabu baada ya kulalamika kuwa na maumivu ya tumbo kiasi cha kulazwa kwenye chumba cha ICU.

Hata hivyo, hali ya msanii huyo inaendelea vizuri na wakati wowote anaweza kuruhusiwa kwenda nyumbani baada ya maumivu hayo kudhibitiwa.



## Rihanna awapagawisha mashabiki wa soka

MREMBO na mwanamuziki wa Marekani, Rihanna, amewashangaza mashabiki wa soka baada ya kuibuka uwanjani kuangalia mchezo kati ya Juventus na Atletico Madrid.

Baadhi ya mashabiki walionekana kupagawa baada ya kumuona mwimbaji huyo akiwa jukwaani huku akivalia jezi na koti maalum la kuzuia baridi.

Rihanna alionekana uwanjani akiwa na pochi ya Louis Vuitton yenye thamani ya paundi Elfu 2000 ambazo ni sawa na milioni 5 za Kitanzania.

## Rapa Gnawi atupwa jela

RAPA Mohamed Mounir maarufu kama 'Gnawi' amehukumiwa kifungo cha mwaka mmoja jela kwa kosa la kutukana Polisi kupitia video aliyoposti kwenye mitandao ya kijamii.

Hata hivyo, imeripotiwa kifungo hicho kimechangiwa na aina ya kazi zake za muziki, hasa baada ya kuachia wimbo wake mpya "Aach al Chaab," aliyowashirikisha Lz3er na Weld L'Griya ambao unazungumzia vitendo vya rushwa vya Serikali ya Moroco.

Serikali imekanusha kukamatwa na rapper huyo hakuhusiani na wimbo wake huo bali ni kutokana na kutoa matusi kwenye mitandao ya kijamii.





## Edo wa Nigeria afariki Dunia

SEKTA ya filamu nchini Nigeria, imempoteza msanii mwingine mkongwe Daniel Uwadiae, anayejulikana kama Edo' ambaye alifariki dunia siku ya Jumanne.

Kwa mujibu wa mtandao wa Legit, kifo cha Edo kimethibitishwa na mtoto wake Ivie Uwadiae ambaye amesema baba yake amefariki baada ya kuugua kwa muda mrefu.


Edo amepata umaarufu nchini humo kwa kuigiza filamu nyingi na kuwavutia mashabiki wengi kutokana na umairi wake wa kuigiza.

## Chioma azungumzia karaha za ujauzito

MKE mtarajiwa wa mwanamuziki wa Nigeria, Davido, ameamua kuelezea namna alivyojisikia wakati akilea mimba ya mtoto wake ambaye amezaliwa hivi karibuni.

Chioma, ambaye anatarajia kufunga ndoa na staa huyo, aliamua kuweka wazi jambo hilo baada ya mashabiki wake kumuuliza maswali katika akaunti yake ya Instagram.

Moja ya video inaonesha mrembo huyo akisema namna alivyojisikia wakati mtoto wake yupo tumboni huku akiwa pamoja na Davido.



SAFU



MIONZI YA SHERIA

# Aliyeanzisha chokochoko ili kuvunja ndoa hupata mgawo?

Na John Juma
0716217615

WATU wengi wamekuwa wakijiuliza ikiwa mmoja wa wanandoa aliyepelekea ndoa kuvunjika kama anastahili mgawo wa mali? Mfano, mwanamke katika ndoa anaanzisha chokochoko makusudi ili ndoa ivunjike apate mgawo wa mali aendelee na maisha yake.

Au mwanamume kwa tabia zake mbaya za ulevi au kutokuwa mwaminifu anapelekea ndoa kuyumba hadi kuvunjika na hapo basi, swali la msingi linapoibuka kuwa tuachane kila mmoja apate mgawo wake, licha ya kwamba kuna mhusika wa kuanzisha sakata.

Siku za nyuma kupitia safu hii , tulichapisha makala iliyozungumzia kuhusu namna ndoa inaweza kufikia tamati au ukomo na pengine kuvunjwa na misingi inayozingatiwa na mahakama katika kugawa mali kwa wanandoa (mke na mume) kwa mujibu wa sheria, hapa nazungumzia Sheria ya Ndoa Sura na. 29, 1971.

Kifungu cha 114 cha Sheria ya Ndoa ambayo hata hivyo Mahakama ya Rufani ilishataka ifanyiwe marekebisho na kuondoa kipengele cha mtoto kuolewa chini ya miaka 14, kwa ujumla sheria hiyo, inaeleza misingi ya kuzingatia wakati wa kugawana mali pale ndoa (baina ya wawili, mke na mume) inapovunjika.

Lakini bado tena katika kifungu hicho, kifungu chake kidogo cha 2(b) kinaeleza kwa kina kuwa kitu kikubwa ambacho kinapaswa kuzingatiwa wakati wa kugawana mali ni mchango wa kila mwanandoa katika kupatikana kwa mali zinazotakiwa kugawanywa.

Yaani kila mwanandoa awe mume au mke kwa nafasi yake ameshiriki kuchangia kwa namna moja au nyingine au kwa kiwango gani katika kufanikisha upatikanaji wa mali husika?

**LA MUHIMU**

Tafsiri ya mahakama kuhusu mchango wa mwanandoa katika kupatikana kwa mali za pamoja: inajumuisha 'mchango wa pesa', majukumu aliyokuwa nayo au nguvukazi': halikadhalika, kazi za nyumbani anazofanya mama au baba mara nyingi hizi hufanywa na mwanamke kama kufua, kupika, kulea watoto, kutunza nyumba na zenyewe zinahesabika kama mchango mkubwa na wa kutosha katika kufanikisha upatikanaji wa mali zote ambazo zitachumwa na mwanaume au mwanamke moja kwa moja kulingana na nani hasa mwenye nguvu ya kipato zaidi.

Mwongozo au tafsiri hiyo inatokana na Shauri la Rufaa maarufu namba 9 la mwaka 1983, TLR 32 kati ya Hawa Mohamed na Ally Sefu. Kimsingi, wenyewe ndiyo msimamo hasa wa sheria, kila linapokuja suala masuala yanayohusika na kugawana mali.

**Hivyo basi, Robert aliamini kuwa mwanamke huyo asingestahili kupata mgawo huo wa mali aliyopatiwa, kwani yeye ndiyo hasa sababu ya ndoa yao kuvunjika.**

Sasa, tukirejea katika msingi wa mada yetu ya leo. Mahakama kupitia kesi ya Robert Aranjo na Zena Mwijuma [1985] TZHC 5; (14 Machi 1985); 1984 TLR 7 (TZHC) inatupatia 'jibu' kama ifuatavyo. Katika shauri hilo Robert Aranjo alikata rufaa Mahakama Kuu ikiilalamikia Mahakama ya Mwanzo na ya Wilaya kwa kumpatia mke wake robo ya mali kama mgawo anaostahili wakati mwanamke huyo ndiye aliyesababisha ndoa yao kuvunjika; huu ni baada ya mke kuamua kuondoka mwenyewe nyumbani kwa sababu anazozijua mwenyewe.

Hivyo basi, Robert aliamini kuwa mwanamke huyo asingestahili kupata mgawo huo wa mali aliyopatiwa, kwani yeye ndiyo hasa sababu ya ndoa yao kuvunjika.

Jaji Maina kama alivyokuwa kipindi hicho, alisisitiza kuwa suala la nani amesababisha ndoa kuvunjika halina uhusiano wowote na suala la nani anatakiwa kupata nini.

Hivyo basi, katika mambo yanayozingatiwa wakati wa kugawa mali pale ndoa inapovunjika swali la nani amesababisha ndoa ivunjike halina nafasi. Na kusisitizia kuwa kinachozingatiwa na kuangaliwa ni kile kilichoelezwa katika kifungu cha 114 cha Sheria ya Ndoa Sura na. 29, 1967 ambacho ni pamoja na mchango wa mwanandoa katika kupatikana kwa kila mali husika.

**ANGALIZO**

Mwisho, kwa kuzingatia hayo kwa wale wote ambao, kwa njia moja au nyingine, walikuwa wanatatizwa na suala husika jibu sahihi linapatikana kupitia maudhui ya makala haya.

Aidha, suala kinzani linaweza kuwapo na hoja zikaibuliwa mfano katika mazingira mengine kama vile sababu au chokochoko zilizopelekea ndoa kuvunjika au masuala ya dai la fidia kwa mwanandoa; lakini siyo kwa kuzuia kupata haki ya gawio la mali iliyochumwa na wanandoa.



KALAMU YA MWALIMU

# Tuzo hizi ni chachu kwa wote walimu, wanafunzi

Na Reubeni Lumbagala

MOTISHA ni kichocheo katika kuchagiza ufanisi na utendaji kazi mahiri na wenye kutoa matokeo chanya. Ni hatua ya kuthamini kazi nzuri iliyofanywa na mtu mwingine katika kuleta mabadiliko chanya ni chachu ya mwendelezo wa mambo bora zaidi ya sasa na baadaye.

Hivi karibuni, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Suleiman Jafo, amekuwa shuhuda wa utoaji Tuzo za Elimu kwa wanafunzi na walimu na shule zilizofanya vizuri kwenye matokeo ya mitihani ya kidato cha sita na darasa la saba kwa mwaka 2019, na kusema kuwa ni chachu ya kuendeleza kazi za kutukuka.

Katika hafla hiyo, Waziri Jafo anatoa fursa kwa wanafunzi waliofanya vyema katika mitihani ya darasa la saba kuchagua shule za sekondari wanazozipenda ili kuendelea na masomo yao.

Anasema kwa wa kidato cha sita Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, iliachiwa wanafunzi wa kidato cha sita ili iweze kuwasaidia kujiunga na vyuo vikuu wavipendavyo. Waziri anasema "Yule kijana Tanzania One nilimsikia anasema anatamani kwenda Shule ya Sekondari Ilboru nitashangaa sana kama hatakwenda huko, hawa ni vijana spesho waambieni wachague shule wanazotaka waende kusoma.

"Naomba niwahakikishie, Rais John Magufuli na serikali anawapenda sana, mtachagua shule zile mnazotaka ninyi kwenda kusoma, Katibu Mkuu shughulikia hilo".

Uhuru waliopewa wanafunzi kuchagua shule na vyuo wanavyovitaka ni motisha kubwa kwani wakati mwingine licha ya kufanya vizuri wanasoma katika shule ambazo hazikuwa matarajio yao na hilo huenda linawavunja moyo kwa sehemu.

Tuzo na zawadi hizo zilizotolewa kwa walimu na wanafunzi zitachechemua kwa kiasi kikubwa ukuaji wa taaluma mashuleni. Wanafunzi na walimu, kila mmoja ataongeza ari katika usomaji na ufundishaji ili kuendelea kupata tuzo na zawadi hizo mara nyingi zaidi.

Ni vyema tuzo hizi zikawa ni jambo endelevu ili kuendelea kujenga shauku kwa walimu na wanafunzi kujituma zaidi. Motisha ni eneo muhimu linalohitaji uwekezaji ili kuongeza tija ya kazi.

Katika sehemu mbalimbali kama maeneo ya kazi, taasisi za elimu, kampuni za umma na binafsi na katika familia utoaji wa motisha ni jambo jema ambalo linahamasisha matokeo chanya na utendaji kazi wenye kasi na viwango. Ndiyo maana katika katika kuziangazia nafasi za tuzo na zawadi katika kuchochea ukuaji wa taaluma kwa shule za msingi na sekondari nchini ni jambo muhimu.

Sekta ya elimu ni muhimu kwa maendeleo ya kila nyanja kama vile kijamii, kiuchumi na hata kisiasa. Kutokana na umuhimu wa elimu, kumekuwa na mikakati ya kuifanya itoe matokeo chanya hasa kwa wanafunzi ambao wapo shuleni kwa ajili ya kusaka maarifa, ujuzi na stadi mbalimbali. Mkakati mmojawapo wa kuchagiza ukuaji wa taaluma ni pamoja na utoaji wa tuzo kwa wanafunzi na walimu kama njia ya kuwahamasisha kujifunza na kufundisha kwa bidii, nidhamu na weledi ili matunda ya elimu hiyo yaweze kuonekana kwa wahusika.

Pamoja na kuwa mwanafunzi anao wajibu wa msingi wa kusoma kwa bidii, kujifunza bila kuchoka na kujituma katika masomo, lakini upo umuhimu wa kuthamini kazi nzuri iliyofanywa na wanafunzi hadi kufanya vizuri katika masomo yao kwa kutoa tuzo na zawadi kwa wahitimu wetu.

Halikadhalika, walimu nao wanao wajibu wa msingi wa kufundisha kwa bidii, kujituma katika majukumu yao, aidha, ipo haja ya kuthamini kazi za walimu kwa kutoa tuzo na zawadi kwa wale ambao masomo yao yamefanya vizuri katika mitihani ya taifa.

Katika hafla hiyo ya utoaji tuzo iliyoratibiwa na Taasisi ya Elimu ya Global Education Link kwa kushirikiana na Baraza Mitihani Tanzania (Necta) na kufanyika jijini Dar es Salaam, Jafo anasema tuzo hizi ni chachu ya ukuaji wa taaluma na kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

"Hizi ni tuzo za kwanza kutolewa na serikali kwani vijana na walimu waliofanya vizuri kwenye mtihani hiyo wanastahili pongezi ili waendelee kufanya vizuri. Tunaamini itaongeza ubora zaidi kwa shule zetu kuendelea kufanya vizuri" anasisitiza Jafo.

Jambo la kipekee katika tuzo hizi ni kwamba wanafunzi na walimu kwa pamoja wanathaminiwa kwani hawa wawili wanategemeana katika kufikia mafaniko ya kitaaluma. Kama walimu watajituma kufundisha kikamilifu na kwa mujibu wa mitaala, huku wanafunzi wakishindwa kujisomea kwa bidii, juhudi za walimu hazitazaa matunda yanayotarajiwa.

Vivyo hivyo kwa wanafunzi ambao wanapenda kusoma huku wakikosa walimu wa kuwafundisha watashindwa kufikia malengo yao ya kufaulu masomoni kwa viwango vya juu. Kwahiyo, ni vyema matokeo mazuri yanapotokea, kila mmoja yaani mwalimu na mwanafunzi kutambuliwa mchango wake katika mafanikio hayo kwani kwa pamoja watakuwa wamewezesha kufikia mafanikio hayo.

Tafakari.

**Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.**

**Maoni: (+255) 764 666349.**

# Baharini kunavyokatis

Na Suleiman Rashid Omar, PEMBA

MOJA ya mazao ya kazi za uvuvi ni uzalishaji wa samaki ambacho ndicho chakula kikuu cha watu wa pwani na maeneo mengine jirani lakini hufikishwa hata ughaibuni.

Wanaoliwa ughaibuni ni kama pweza, majongoo maji, kamba kochi na lobsta , jodari na jamii nyingine za change.

Licha ya kwamba ni chanzo cha ajira kwa vijana, wazee na kina mama wengi ambao hufanya biashara ya kukaanga na kuuza samaki iwe mijini na vijijini, kwa kiasi kikubwa ni kazi yenye shuruba.

Ukitaka kujua uzuri na umuhimu wa uvuvi nenda kwenye minada ya samaki na uone mkusanyiko wa wateja unavyohaha kutafuta kitoweo lakini pia wanavyo wasubiri wavuvi ili wawaletee samaki.

Mambo yanayokuwa magumu wakichelewa kwani wapo wanaotoka umbali mrefu baharini, mkondoni na cha muhimu cha kujua ni kuwa kazi hii ya uvuvi ni roho mkononi kwa vile wapo wengi walioangukia baharini na kupoteza maisha.

Wakati ukitafakari uzuri na ugumu wa kazi ya uvuvi sambamba na utamu wa kitoweo samaki, kinavyotakasa nafsi ukumbuke kuna familia kadhaa hapa kisiwani Pemba zinazoumizwa na machungu ya kuuguza majeraha ya mioyo yao kwa kupoteza ndugu zao walio kwenda baharini kuvua.

**SAA 48 BAHARINI**

Nipashe ilisafiri hadi eneo la Shumba mjini huko Wilaya ya Micheweni kisiwani Pemba ambako hivi karibuni wavuvi nane walizama na watatu walifariki na kuacha wajane na watoto kwenye maisha magumu, kisa kilichotokea wakiwa wanasaka samaki.

Katika mazungumzo mvuvi Rashid Othuman, anasimulia mkasa huo aliompata akiwa anakumbukia alivyoteseka baharini saa 48 . Anasema ni siku nne alizoishi baharini akiwa nusu duniani na nusu nyingine akiwa ndani ya bahari.

Anaeleza kuwa hizo ni miongoni mwa changamoto wanazokutana nazo wavuvi, akisisitiza kuwa ameishi baharini siku nne akipigwa na jua mchana lakini pia bila kula, kunywa wala kusinzia mchana na usiku.

"Jua ni kali, hakuna kulala tukiwa nusu mwili umezama ndani ya bahari na mwingine uko duniani. Mawimbi, upepo na baridi vikawa ni sehemu ya maisha yetu kwa siku hizo. Ingawa njaa tulizihisi hatukuweza kupata chakula," anasema Othuman.

**CHANZO CHA MKASA**

Othuman anasema maji yaliwateka baada ya wimbi kubwa kutua juu ya chombo chao na kuwasukuma hadi mkondoni. Mkondo ni sehemu yenye maji mengi na kina kirefu.

"Baada ya kutupwa mkondoni



Ni kazi ngumu kuingia baharini lakini wavuvi wanajitolea maisha yao kuvua. **PICHA: MTANDAO**



Wavuvi wanaitaja bahari kuwa sehemu yenye kitisho na hofu muda wote. **PICHA: MTANDAO**

nguvu zilituishia tukawa hatuna ujanja maji yakatupeleka tusikokujua huku mawimbi hakuna dakika ambayo yalituhurumia yalitulowesha kila muda tukawa kama jiwe. Tulidonolewa na samaki wadogo miguuni muda wote. Lakini ni ajabu hatukuhisi maumivu utadhani miguu sio yetu," Othuman anakumbukia kwa uchungu.

Anasema uchungu walioupata hawawezi kuusahau kwani walisota baharini kwa muda wa siku nne akiwa na wenzake wanne, lakini mmoja wao alifariki. Hayo yalijiri baada ya boti yao kupigwa na dhuruba kali ya wimbi makubwa.

**HAKUNA UZOEFU**

Mvuvi mwingine kwenye janga hilo ni Ali othuman, licha ya kujisifu kuwa yeye ni mvuvi mwenye taaluma kubwa kutokana na kuishi baharini japo hakwenda shule, anaamini ni mbobezi kwani ametumia muda wake wote katika kujifunza uvuvi tokea akiwa mdogo kwa kwenda kuvua kwa mishipi kwa kutumia miguu kwenye mito midogo na kila alivyokua ndivyo alivyo sogea baharini baadae alipofikia miaka 20 akamua kuingia baharini kwa kutumia ngalawa.

**DHIKI KUU**

Mbobezi Ali Othuman anasema:"Mimi katika maisha yangu haya ya uvuvi ambayo ndiyo sehemu kubwa ya shughuli zangu nimeshazama baharini mara tano na zote zote nimeokolewa"

Licha ya kwamba cha moto alikiona lakini safari hii kukaa baharini siku nne halikuwahi kumtokea kwani alikuwa anaokolewa baada ya saa kadhaa, anaeleza.

"Mara ya kwanza nilizama saa 8:00 mchana nikiwa umbali wa mita takribani 80 kutoka bandarini, haikuchukua muda ilipofika saa 10 walikuja wavuvi wenzetu tukaokolewa," anaongeza Ali.

Anasema yalipomkuta hayo alipata hofu kidogo ilihali aliendelea kazi na baadaye hofu ilimtoka na kuchapa kazi kam kawaida, japo haikuchukua muda mara ya pili baada ya mwaka moja kupita

# sha maisha ya wavuvi



tangu kuzama mara ya kwanza ngalawa yake ilipinduka akiwa kwenye mkondo (maji mengi na marefu) lakini haukupita muda akaokolewa.

Anasema mara ya tatu akiwa anendelea na kazi yake ya uvuvi katika mwambao wa Songo Songo kwenye bahari ya Tanzania Bara majira ya saa 2:00 asubuhi chombo chao kilizama na hivyo kubaki kwenye maji hadi saa 12 jioni.

"Tulikaa ndani ya maji makubwa saa 10 hadi walipotokea wavuvi wakatuokoa. Hii mara ya nne tulikuwa na ngalawa kwenye mkondo nikazama ngalawa ikakokotwa na maji tuliogelea mpaka saa 12 tukafika bandarini Tumbe "anasema Ali.

**PWANI YA KENYA**

Ali anasema: "Mara hii ya tano tuliokoka tukiwa Kenya. Kutoka Pemba hadi bahari ya Kenya tulikutana na msukosuko, katika maisha yangu sitasahau kwani nikiulizwa tamu na chungu ya uvuvi yote nayasamehe ila hii hapana. Nikiyazungumzia basi hata moyo wangu huharibika kwani tulikuwa katika shida kubwa mno."

Akisimulia anasema waliondoka bandarini saa 9:30 usiku kwa ajili ya kwenda kuvua lakini wakitafuta chombo walikipata na ilipofika saa 10 waliingia baharini kwa ajili ya kazi.

Wakati wakiwa baharini ghafla nahodha aliwaamuru kuvuta nanga ili waondoke sehemu waliokuwa ambapo ni umbali wa kama maili 200 kutoka bandarini. Hata kabla ya kutiia maagizo ya nahodha, ghafla liliibuka wimbi kubwa mithili ya nyumba ya ghorofa lilisimama na nakuja upande wao kwa kasi ya ajabu

"Ilikuwa tabu bila hata ya kulikwepa lilipiga boti yetu ikapinduka nasi kuzamishwa kwenye maji. Tukiwa tunatapatapa mara niliona boti yetu imeibuliwa na wimbi kwa mbali inaelea, nikawaambia wenzangu tushapona boti yetu ile tuifuate tukaifuata tulipoifikia ilikuwa inaelea kimgongomgongo tukajitahidi kuigeuza na kufanikiwa lakini chombo chote kikawa kimejaa maji," anasema Ali.

Anasimulia kuwa mara baada ya chombo chao kupigwa na wimbi na kuzama nanga haikuonekana kabisa nao wakawa wanatapatapa hawajui la kufanya huku mawimbi yakiwapiga kuwazamisha na kujitahidi kuibuka shida iliyowakumba kwa takribani saa mbili.

Waliingia vivyo hivyo wakajikuta wapo watatu mwenzao wanne ikiwa hawamuoni ambae ni omar Ali Hassan.

"Lakini kwa mbali nikamuona nikamwita ila alianza kupoteza nguvu nikaenda kumchukua hadi kilipo chombo nikamkamatisha ili arukie ndani ila alishindwa ghafla likapiga wimbi tukapoteana tena."

Anakumbusha kuwa alipozama alikuja juu na kumtafuta ila jitihada za kumsaka zilikwamishwa na wimbi zito wakati huo walikuwa wamekwisha ingia kwenye boti iliyojaa maji ikiwa inapelekwa na mkondo mkubwa wa maji wakiwa na hawana tanga ,upondo wala kafi na mashine au injini ilikuwa haiwezi kuwaka.

Na hapo wakajua kuwa mwenzao tayari amewatoka anasimulia jinsi walivyo ishi ndani ya siku nne hizo wakiwa baharini bila kula kunywa au kufanya chochote walichofanya walikata vipande vya mishipi walio kuwa wakivulia ambao ilibakia kwani vitu vyao vyote ni kama vilipotea .

Anasema walipata hasara ya Shilingi 3,000,000 ikiwa ni pamoja na mishipi chombo chao dira cha kuwaongozea wakiwa baharini GPS ambavyo walikuwa nazo mbili, mishipi gunia nzima na vitu vingine vingi ambavyo vyote vilipotea.

Boti ilipoibuka ilikuwa imejaa maji nao walishindwa kuyatoa huku ikielea wakiwa wamekaa maji yakiwa yanawafika kwenye tumbo kila mara walilowa kwa kupigwa na mawimbi.

'Sisi tuliamua kujifunga ndani vya boti hivyo hivyo tikitarajia kuwa tukifa boti ikifika juu na maiti zetu zionekane ndani ya boti hivyo kilamoja alijifunga kamba madhubuti ikawa wimbi linapiga kurusha na kutua ila hatutoki ndani ya boti.'anasema.

"Nilijifunga mpira wa mashine ya boti kiunoni ukanikaa kisawasawa nikajua hapa sitoki" anasema Ali.

**KUOKOLEWA**

Ali Rashid anakumbuka kuwa wakati wakiwa majini hawajui waendako wala watokako, lakini bila kukata tamaa kwasiku ya tatu wakiona meli kubwa zikiwapita karibu lakini hazikushughulika nao hadi siku ya nne ambapo walifanikiwa kuokolewa wavuvi wa Kenya.

Muuvi Ali Hassan Kombo , naye anaelezea mambo yalivyowatisha baharini akiiambia Nipashe kuwa siku waliyokwenda baharini kuvua tangu wanaondoka upepo ulikuwa mkali hali iliyokuwa ngumu ila kwa kuwa ni kazi yao waliona waende ila hali ilikuwa inatisha.

Anasema walipofika umbali mita 250 kutoka bandarini mbali na mkondoni walitia naga ambapo hapo ndipo walipokutana na kadhia hiyo ya kuzama maji yakiwa na kina kwa kwenda chini kama maili 18 kutoka baharini hadi bandarini

Anaeleza kuwa siku hiyo maji yalikuwa makali kutokana na upepo na mawimbi yalikuwa makubwa na hivyo kuwafanya kuwa katika hali ngumu kwa kurushwa kutoswa majini kiasi cha kuhofia kiwa wasingeokolewa.

Kombo alisema katika uzoefu wake wa uvuvi tayari alishawahi kuzama mara tatu baharini lakini aliweza kuokolewa na hivyo kumpa matumaini na akuendelea na kazi yake ya uvuvi ambayo imekuwa ikimpa fedha za kutunza familia yake ya watoto sita na mke mmoja.

**WENGINE WALIKUFA**

Kombo anaeleza kuwa mbali ya chombo chao pia kulikuwa na wenzao ambao chombo chao hakikuibuka na idadi yao walikuwa wanne.

Anawataja wenzao hao kuwa ni Salum Abdalla Ali Kombo Fakih Mcha, Mwalimu Bossi Faqih na Omar Kombo Faqih ambao walikuwa kwenye chombo kimoja ambacho hakikuonekana kikisadikiwa kuwa kimezama na wavuvi hao kufariki. Wavuvi hao walishukuru jinsi walivyo weza kuokolewa wakasaidiwa hadi kufika nyumbani kwao ila bado halizao ni ngumu kwani miili yao iliumia kwenye bahari na hawajaweza kufanya harakati zao za maisha ila wanaendelea kuishi.

Wanaomba serikali kuwatafutia njia mbadala ya kuweza kujitafutia maisha yao wachane na kazi ya uvuvi ambayo imekuwa mtihani mkubwa kwao, na kwa ujumla wavuvi wote

Wamewataka walezi na wazazi kuwasimamia vyema watoto wao na kuwasaidia wasome ili wajiajiri au kuajiriwa na waachane na kazi ya uvuvi kwani ni hatari na inawaweka wavuvi roho mkononi muda wote.

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 22 00)

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | 2 | | | | | | ■ | 3 | ■ | 4 | ■ |
| | ■ | | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | 5 | | | | |
| 6 | | | | 7 | | 8 | 9 | ■ | | ■ | | ■ |
| | ■ | | ■ | | ■ | 10 | | | | | | ■ |
| 11 | | | 12 | | 13 | | | ■ | | ■ | ■ | 14 |
| | ■ | 15 | | | | | ■ | ■ | | ■ | ■ | |
| ■ | 16 | ■ | 17 | | | ■ | 18 | | | | | |
| 19 | | | | | | 20 | ■ | ■ | | ■ | ■ | |
| ■ | | ■ | | ■ | 21 | | | 22 | | ■ | ■ | |
| ■ | 23 | | | | | | ■ | | ■ | 24 | ■ | |
| ■ | | ■ | ■ | ■ | | ■ | 25 | | | | | ■ |
| 26 | | | | | | ■ | ■ | | ■ | | ■ | ■ |
| ■ | | ■ | ■ | ■ | ■ | 27 | | | | | | |

Dondoo: Kulia
1. Kuala Lumpur ni mji mkuu
5. Kazi ya msanii
6. Kisiwa cha Unguja na Pemba
10.Tunda lenye miba miba
11.Mtawala
15.Kwa ajili ya
17.Toka jasho
18.Dakitari
19.Mwanafunzi wa Upadri
21.Amri, hukumu
23.Kitu cha kuthibitisha ushahidi
25.Chakula cha nyuzi nyuzi
26. Dhana ya kazi
27. Ahadi ya kumdhamini mkopaji

Dondoo: Chini
1. Wimbo
2. Jiji lenye meya Sadiq Khan
3. Wingi wa neno jaribio
4. Baina ya
7. Japokuwa
8.Kuwa wa awali
9.Maoni
12.Mji mkuu wa Niger
13.Rais mstaafu wa Nigeria
14.Hutumika kuhifadhia maji
16.Imara
20.Fuatisha
22.Nyongeza
24.Mnyama alindaye makazi

## Jibu toleo lililopita

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Z | I | M | B | A | B | W | E | ■ | ■ | P | ■ | T |
| A | ■ | W | ■ | D | ■ | I | ■ | M | T | I | M | A |
| M | K | A | T | A | B | A | ■ | A | ■ | N | ■ | M |
| A | I | N | I | A | ■ | N | ■ | L | ■ | G | ■ | A |
| N | A | Z | I | ■ | S | A | R | A | F | U | ■ | D |
| I | D | A | ■ | ■ | H | ■ | ■ | W | ■ | ■ | ■ | U |
| ■ | A | ■ | M | T | U | N | G | I | ■ | K | ■ | N |
| S | ■ | ■ | S | ■ | K | ■ | A | ■ | U | A | N | I |
| W | A | T | U | K | U | T | U | ■ | T | A | A | ■ |
| A | ■ | ■ | M | ■ | R | U | N | G | U | ■ | N | ■ |
| L | A | P | A | ■ | U | M | I | A | ■ | D | A | U |
| A | ■ | ■ | R | ■ | ■ | B | ■ | R | ■ | ■ | S | ■ |
| ■ | M | P | I | N | G | O | ■ | I | S | H | I | A |

MAKALA

## TUMBAKU HII

# Tani milioni 7 zawadodea wakulima, walia umaskini

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

SERIKALI safari hii imeichagua tumbaku kuwa moja ya mazao ya kimkakati na inaitaja kuwa zao kipenzi, linaloongoza kuingizia nchi fedha za kigeni.

Tumbaku inalimwa katika wilaya nyingi za mikoa ya Shinyanga, Geita, Tabora, Songwe, Katavi, Rukwa, Iringa, Singida, Mbeya, Kagera na Mwanza.

Taarifa za Benki Kuu (BoT) za Januari mwaka huu zinaonyesha kuwa tumbaku ni ya kwanza iliingiza wastani wa dola milioni 222.6 ikifuatiwa na korosho dola milioni 196 .5.

Wakulima wa tumbaku ni mahodari na wanajitamba kuwa wamezingatia kilimo cha kisasa na kuzalisha takribani kilo 750 kwa hekari lakini hawana mnunuzi.

Wakifafanunua zaidi wanasema kuzingatia utaalamu na maelekezo ya maofisa ugani uzalishaji kwenye hekari moja inayotakiwa kutoa kilo 560, mkulima anapata hata kilo 750.

Licha ya wakulima kutumia teknolojia ya kisasa wanakabiliwa na changamoto lukuki kila wakati kutokana na madaraja ya tumbaku na namna inavyonunuliwa, soko lake kutoeleweka pamoja na wakulima kupangiwa kiasi cha kuzalisha, huku uzalishaji ukishuka kila mwaka

Mwaka huu wakulima wamebaki njia panda na kuiomba serikali kuwatafutia soko la kilo milioni 6.5 za tumbaku ya ziada ambayo haijanunuliwa mpaka sasa.

Shehena hiyo iko kwenye maghala ya kuhifadhia tumbaku na kiasi kingine nyumbani huku wakulima wakiwa hawajui hatima ya tumbaku hizo.

Wakizungumza kwenye mahojiano maalumu na Nipashe wakulima wa zao hilo walisema wamewekeza fedha na nguvu kwenye zao hilo ili kujikwamua kiuchumi na kujiletea maendeleo na juhudi zao zinakwamishwa na ukosefu wa soko.

**KILIO CHAO**

Mmoja wa wakulima hao Kulwa Shoto, anasema kuzalishwa kwa tumbaku hiyo ya ziada kumetokana na kuzingatia na kufuata ushauri wa maofisa kilimo na ugani, matumizi bora ya pembejeo, kupanda kwa nafasi na matumizi ya viuatilifu na kulima kilimo bora na chenye tija .

Sababu nyingine anayoielezea Shoto ya uwepo wa tumbaku ya ziada ni kiasi kilichowekwa stoo ni kuzingatia uzalishaji kwenye hekari moja inayotakiwa kutoa au kuzalisha kilo 560 wakati mkulima akitunza vizuri kwa kufuata maelekezo ya watalaamu na hali ya hewa ikawa nzuri lazima tumbaku izidi na wanauwezo wakuzalisha kilo 750 kwa hekari moja .

"Kununuliwa kwa tumbaku yangu kungeniwezesha kupata chakula , kulipa ada za watoto , kupata fedha ya kujikimu na shughuli za maendeleo. Lakini yote hayo yamekwama kutokana na kutokununuliwa kwa tumbaku hii, anasema Shoto.

Emanuel Nyambi mkulima na mmoja wa viongozi wa chama cha ushirika cha msingi cha Kipalapala AMCOS kutoka Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama anaongeza kuwa wanaiomba serikali iwasaidie kwa jitihada mbalimbali za kupata soko la tumbaku hiyo ili waondokane na hasara.

Tumbaku hiyo ambayo iko kwenye maghala ya kuhifadhia tumbaku ya AMCOS na nyingine imehifadhiwa majumbani ziko kwenye hatari ya kushambuliwa na wadudu na ubora kupotea.

Anasema ni tatizo kwa kuwa uhifadhi wa zao hilo ni mgumu na unahitaji fedha nyingi ambazo mkulima hawezi kumudu kuwa nazo.

"Msimu mpya wa kilimo umeanza, wakulima wameingia msimuni wameanza kulima na kupanda tumbaku wakati nyingine bado iko ndani haina mnunuzi na mpya ikiwa tayari, kampuni za ununuzi hayawezi kuchukua ya msimu uliopita jambo hili lilishatokea miaka ya nyuma tulipata hasara wanunuzi waligoma kununua mazao ya msimu uliopita "anasema Nyambi.

Anaiomba serikali isimamie na kuliangalia tatizo hili kwa umakini mkubwa huku ikiwasaidia kwa kuwa kuna wakulima wameingia shambani msimu huu hawajui nani ananunua tumbaku iliyohifadhiwa ghalani.

Ni kwasababu kampuni ya Tanzania Leaf Tobacco (TLTC) iliyokuwa wanafunga nayo mikataba ya kuuza na kununua ikiwamo kupangiwa kiasi cha kuzalisha kujitoa kununua zao hilo msimu huu kwa kuwa bado ni shida na ni changamoto kwao .

Akizungumzia tatizo hilo mkulima Scholastica Nyanda, mama mwenye watoto saba kutoka Ulowa wilayani Kahama anasema aliingia kwenye kilimo cha tumbaku kwa lengo la kujikwamua kiuchumi.

Nyanda anasema miaka ya nyuma alikuwa akilima tumbaku na baada ya kuuza fedha iliyopatikana waliweza kununua mahindi na mahitaji mengine ya msingi ya familia yao pamoja na kuwalipia akiwamo mtoto wake aliyemaliza kidato cha sita anayesoma chuo pamoja na kuweka akiba hali ambayo kwa sasa imekuwa ndoto .,

**BEI MASOKONI**

Wastani wa bei ya tumbaku kitaifa ni Dola 1.72 msimu wa 2018/2019 lakini kuna baadhi ya maeneo masoko yalisimamia wastani wa Dola 1.5 , huku tumbaku ya ziada iliyobahatika kuuzwa ikiuzwa kwa wastani wa dola 1.16 tofauti hiyo ni kubwa kwa mkulima kutokana na mikopo ya pembejeo na ya mabenki aliyonayo na hivyo kumsababishia hasara .

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU) Emanuel Cherahani, anaiomba serikali iziangalie kwa karibu changamoto zinazolikabili zao la tumbaku kwa sasa ili zitatuliwe kwa haraka la sivyo hali inazidi kuwa mbaya kutokana na kampuni kuzidi kushusha uzalishaji.

Cherehani anasema athari ya tatizo hilo la kukosekana kwa soko la tumbaku ya ziada ni kuporomoka kwa uchumi wa wakulima wote na mtu mmojammoja sambamba na kupungua kwa kipato cha halmashauri zinazolima tumbaku.

**UFAFANUZI WA BODI**

Mkurugenzi wa Bodi ya Tumbaku (TTB), Stanley Mnozya anasema kilo za mkataba zilikuwa kilo milioni 57, mpaka msimu unafungwa Agosti mwaka huu walikuwa wamenunua kilo milioni 60.7

Baada ya tathmini mwezi wa Julai na Agosti, walibaini wakulima wamezalisha tumbaku zaidi ya kilo milioni 12.5 nchi nzima na baada ya hilo, bodi iliwasilisha maombi kwa kampuni mbili ya ununuzi yaliyopo nchini ili ziweze kununuliwa zaidi au zilizo nje ya mkataba.

Tumbaku zilizo nje ya mkataba haina sheria ya kuilazimisha kampuni iinunue kwa mujibu wa Mnozya na kwamba kampuni mbili zilikubali kununua na mbili ziligoma, kampuni ya Alliance One Tobacco ilikubali kununua kilo milioni 4.2 na Premium kilo milioni 2.1 zikikubali kununua kwa bei pungufu ya dola 1.16, wakati tumbaku ya mkataba ilinunuliwa kwa wastani wa dola 1.72 .

" Tumbaku ya ziada mkulima anauza kwa bei ya chini na ya hasara kwa kuwa hailingani na gharama za uzalishaji kwa kilo ya tumbaku kwa kuwa haina sheria ya kumbana na kumlazimisha mnunuzi na ni ya kuomba " anasema Mnozya.

Maoni ya Emanuel Nyambi kwa Waziri wa Kilimo, anamtaka aharakishe kupata ufumbuzi wa suala hili ili wakulima waweze kuondokana na hasara ikiwa ni pamoja na kutafuta masoko kupitia kampuni za ununuzi wa tumbaku ndani na nje ya nchi na ili wakulima wa zao hilo waweze kupata masoko ya uhakika .

**ANGALIZO LA MBUNGE**

Naibu Waziri wa Ujenzi na Mawasiliano, Elias Kwandikwa ambaye pia ni mbunge wa Ushetu aliwahi kulizungumzia suala hilo kipindi cha nyuma kulipotokea changamoto kama hiyo .

Kwandikwa alisema mfumo uliopo ni wa kinyonyaji na uliwekwa kwa misingi ya unyonyaji ikiwamo mikataba na makubaliano ya mnunuzi na mkulima yasiyo na tija kwa mkulima ikiwamo mhusika kulima kwa kupangiwa kiasi cha kuzalisha kulazimishwa kukopeshwa jambo ambalo halina tija kwa mkulima .

Hivyo mfumo utazamwe upya kuanzia kwenye uzalishaji mpaka malipo na kuondolewa kwa masharti yasiyo na tija na kuongeza kuwa athari ya kukosekana kwa soko la tumbaku hiyo ni kubwa.



Mkulima wa tumbaku akiwa kazini .**PICHA : MTANDAO.**

HABARI KIMATAIFA

# Kasi ya mauaji Congo yaongezeka

**KINSHASA , Congo**

KUNDI hatari la wapiganaji limewauwa jumla ya watu 27 katika mauaji ya kinyama yaliyofanyika mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo juzi Jumatano.

Idadi hiyo ni kwa mujibu wa polisi. Ikitoa taarifa mpya ya idadi ya vifo, ilisema wahanga walikatwa mapanga katika eneo la Oicha, karibu kilometa 30 kutoka mji wa Beni.

Polisi iliandika kwenye ukurasa wa Twitter kuwa kuna miili 27 kwenye chumba cha kuhifadhi maiti cha hospitali ya Oicha, na kufikisha 107 idadi ya watu waliouawa ndani na karibu na mji wa Beni tangu Novemba 5 mwaka huu.

Mauaji mengi yamefanywa na ADF, kundi la waasi ambalo limeendesha harakati zake katika maeneo ya mashariki ya Congo tangu miaka ya 1990.

Mauaji hayo yamezusha maandamano dhidi ya jeshi la kulinda amani nchini Congo - MONUCO. Juzi mabalozi wa Uingereza, Canada, Uswisi na Marekani waliandika barua ya pamoja wakilaani mashambulizi dhidi ya MONUSCO

*DW*



Wanawake wakiwa kwenye harakati nchini Sudan. **PICHA: AFP.**

# Wanaharakati wanawake washambuliwa, kuuawa

**LONDON, Uingereza**

WANAHARAKATI wa haki za wanawake wameendelea kudhulumiwa kingono, kutishiwa, kudhalilishwa na hata kuuawa, ripoti ya Shirika la Kimataifa la Amnesty International, imesema.

Shirika hilo lilisema katika ripoti yake kwamba watetezi wa haki za binadamu mara nyingi wanapokea vitisho na mashambulizi ambayo yanahusiana na kazi yao ya kupigania haki za wanawake na usawa wa kijinsia.

Katika ripoti hiyo ya kuadhimisha siku ya kimataifa ya watetezi wa haki za wanawake, Amnesty ilisema wanaharakati hao wameendelea kupokea vitisho, kudhulumiwa kingono, kudhalilishwa na hata kuuawa.

Katibu Mkuu wa Amnesty, Kumi Naidoo alisema, "wanaharakati wa masuala ya haki za wanawake wanashambuliwa kwasababu ya kazi wanayoifanya. Vitisho hivi ni vikubwa kwa wale wanaokabiliwa na aina zote za unyanyasaji, kwa mfano ukiwa mwanamke na unatoka jamii ya wachache, mtu wa makabila ya asili, maskini, unapaswa kupambana zaidi ili sauti yako isikike na wale walioko madarakani".

Licha ya maendeleo katika harakati za wanawake ambayo yamepata nguvu kuliko hapo awali, bado wanaharakati wa kike wanakabiliwa na shinikizo katika miaka ya hivi karibuni kutoka kwa wanasiasa, viongozi wa kidini na makundi yaliyo na vurugu yanayosambaza "siasa za kikatili".

Ripoti hiyo iliyopewa kichwa cha habari "Kukabiliana na mamlaka, kupinga ubaguzi, wito wa hatua zaidi za kutambua na kuwalinda wanaharakati wa haki za wanawake".

Aidha, ilitolea mfano Poland ambayo baadhi ya wanaharakati wa kike wamekabiliwa na mashambulizi katika mazingira ambayo ubaguzi wa rangi na chuki dhidi ya wahamiaji vimeongezeka.

Bahrain na Misri, udhalilishaji kingono unatumika kama aina ya mateso ili kuwanyamazisha wanaharakati wa kike.

Wanawake pia wanakabiliwa na ukatili wa majumbani na unyanyasaji kulingana na dhana za kimila ikiwamo vitisho vya talaka au kutenganishwa kwa nguvu na watoto wao.

Vile vile wanaharakati wa wanawake mara nyingi wanakumbwa na kampeni za kupigia debe kushambulia tabia zao ambazo Amnesty wanasema zimeundwa makusudi ili kujenga uadui dhidi yao.

Mfano ni waziri wa zamani wa mambo ya ndani wa Italia Matteo Salvini ambaye alimdhihaki Carola Rackete, nahodha wa meli ya uokozi ya Sea-Watch 3, na kufuatiwa na wengine waliochochea unyanyasaji kijinsia na mwonekano.

Amnesty International inatoa wito wa wanawake hao kutambulika na kulindwa kutokana na kazi ya ujasiri wanayoifanya kuboresha maisha ya jamii zilizotengwa.

*DW*

## Wanaharakati nchini Sudan wafuta chama cha Al Bashir

**Khartoum, Sudan**

MZOZO wa Sudan umechukua sura mpya na sasa chama cha rais wa zamani Omar al-Bashir kimefutiliwa mbali.

Sheria ilipitishwa nchini Sudan ya kuvunja chama cha rais aliyeng'olewa madarakani Omar al-Bashir ambaye alichukua mamlaka 1989 kwa mapinduzi na kuliongoza taifa hilo kwa takriban miongo mitatu, hadi alipoondolewa kwa vuguvugu la maandamano ya upinzani Aprili mwaka huu.

Mamlaka inayoongoza kipindi cha mpito nchini humo pia imeondoa sheria ya umma ambayo ilitumiwa kudhibiti mienendo ya wanawake.

Hatua zote zimejibu madai muhimu ya vuguvugu la waandamanaji, ambayo yalilenga kuvunja utawala wa Bashir.

Sudan kwa sasa inaongozwa na utawala unaojumuisha jeshi na baraza la kiraia pamoja na baraza mawaziri la raia linaloongozwa na Waziri Mkuu, Abdalla Hamdok.

Kuvunjwa kwa chama tawala cha Bashir cha National Congress Party (NCP) inamaanisha kuwa mamlaka zinaweza kuhodhi mali za chama hicho .Sheria ilithibitisha kuwa kamati itaundwa kutekeleza hatua hiyo.

Hii inafanyika ili waweze kurejesha utajiri ulioibiwa wa watu wa Sudan, alisema Hamdo katika ujumbe wake wa twitter.

Sheria hiyo pia inasema "hakuna nembo yoyote ya utawala au chama itakayoruhusiwa kuhusika katika shughuli yoyote ya kisiasa kwa miaka 10 .

Msemaji wa Muungano wa Wasomi wa Sudan, kikundi cha waandamanaji kilichompindua rais al-Bashir, aliiambia BBC kuwa huu ulikuwa ni wakati wa kihistoria.

"Huu ni wakati wa ahueni, kwasababu kila mtu nchini Sudan ameathiriwa vibaya kwa namna moja au nyingine na utawala," alisema msemaji Samahir Mubarak.

Hata hivyo, mchambuzi wa siasa kikanda, Mohammed Issa, alisema ilipotokea hali kama iliyoikumba Sudan chama tawala kilichokuwa madarakani kinapinduliwa na kwamba hatua ya kukivunja haina maslahi kwa mustakabal wa Sudan.

"Hatua iliyochukuliwa na viongozi wa mpito kujenga utengamano haina maslahi katika kujenga utengamano wa Wasudan. Ilitarajiwa kwamba kungekuwa na ujumuishaji wa makundi yote katika siasa za nchi kwa ajili ya mustakbal.", aliiambia BBC.

Aliongeza:' Kuvunjwa kwa chama cha National Congress , kinawaacha viongozi na wafuasi wa chama kile na washirika kama vile wafuasi wa kundi la Janjaweed bila uwanja wa kuelezea maoni yao ya kisiasa, na hali hiyo inaweza kuwafanya waelezee hisia zao kwa njia ya vita na uasi".

**BBC**

# HADITHI

# Jumba Jekundu-29

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.
Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.
Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**




Kadili alishtuka. Edina mwenyewe aliuona mshtuko wa Kadili ukiwa dhahiri. Alijua baada ya kuachiwa kwenye jumba jekundu alikuwa yuko salama. Alianza kuwa na mashaka ya usalama wake pale tu aliposikia Edina ametoroka kwa mumewe.

"Bado ulikuwa kwenye mahesabu ya mama na kundi lake, ilikuwa uuawe ama kwa ajali, sumu au kitu chochote kile, lakini isijulikane kama yeye ndiyo amesababisha kifo chako. Kingekuwa ni kifo ambacho hata mimi nisijue kuwa yeye amehusika kwa sababu kama ningejua ningelianzisha na hakungekalika, au na mimi ningekunywa sumu, kitu ambacho mama hakutaka kitokee.

Na kifo chako kiliandaliwa ili mimi niweze kukubali kuolewa kwa sababu mama aliamini kuwa wewe ndiye unayesababisha mimi nikatae mpango wake."

Kadili alibaki ameduwaa tu. Hakuna na nguvu za kusema neno lolote. Hakujua kuwa tangu alipotoka kwenye jumba jekundu alikuwa akitembea na kifo mkononi.

Na kwa mara nyingine tena, msababishaji ndiye aliyemuokoa.

"Kuna mtu wangu kati ya wafanyakazi wa mama ambaye kila kitu kikifanyika au kusemwa, ni lazima anipe taarifa za siri. Akaniambia jambo hilo. Kwanza niliwaza kuja kwako, nikutafute nikikupata nikuhamishe hapo ukakae sehemu nyingine, lakini nikaona nitaipa shida na wasiwasi familia yako.

Lakini pia hata huko unakokwenda mama alikuwa na mkono mrefu, ungeweza pia kujulikana. Nikaamua kuolewa ni kukunusuru, lakini nilikuwa na langu moyoni." Edina aliyasema maneno hayo kwa namna ya simanzi. Wakati Kadili akiwa kama amepigwa na shoti ya umeme, au kupigwa ganzi Edina aliendelea.

"Nilipokubali niliona sasa utaendelea kuwa hai mtu wangu, kwani tayari nimempumbaza mama, nikaolewa na Dk. Kapilima kwa sherehe kubwa sana kama binti wa kitajiri na ilipoisha nikaanza maisha ya mke na mume.

Kwa muda mfupi tu nilichokuja kugundua kuwa mimi nilikuwa simpendi, yeye alinipenda, lakini hakuwa mume mwema, utajiri wake na umaarufu ulimfanya kuendelea kumiliki wanawake wengi sehemu mbalimbali akiwa amejengea nyumba, kuwapangisha nyumba na vyumba pia. Anaweza akaondoka nyumbani wiki nzima akasema yuko kikazi. Mimi ni binti wa kitajiri. Nikamwajiri mpelelezi binafsi mmoja amchunguze kila anakokwenda na aniletee taarifa. Alikuwa na kila kitu hadi kamera. Wiki mbili tu akaniletea mrejesho.

Ilikuwa nusura nizimie.

Ndipo nilipogundua kuwa sijapata ila nimepatikana. Na hata mimi mwenyewe lengo langu kuolewa halikuwa kuishi na yeye Dk. Kapilima, bali ilikuwa ni kukuokoa wewe na akilini mwangu nilijua nini nitafanya. Lakini kabla ya kufikiria hilo, akanitibua akili yangu, hasira zinanipanda." Wakati Edina akiendelea alionekana kama vile hasira zinaanza kumpanda, mikono ikitetemeka.

"Aliporejea aliposema amekwenda kwenye safari zake, nilimuuliza akasema ni kweli alikuwa safarini, nikamuonyesha picha za video za mambo yote aliyokuwa anayafanya. Alichokifanya ni kunipiga, akanikaba nusura anitoe roho, ananinyang'anya simu ambayo nilikuwa nimehifadhi video hiyo ili kuharibu ushahidi.

Nilichokifanya baada ya hapo nikamtoroka." Alipomaliza alishusha pumzi kana kwamba ametua mzigo mzito aliokuwa umeubeba.

Kadili alimuangalia kwa jicho la huruma. Edina akatoa macho yake yaliyokuwa yakiangaliana na Kadili na kuyakwepesha.

Kadili alinyanyuka na kumfuata karubi Edina. "Kumbe maisha yangu yalikuwa mikononi mwako. Umekuwa mlinzi wangu kabla sijatekwa nilipoingizwa kwenye jumba la mama yako, nilipotoka hadi nilipoendelea kuwa nyumbani. Naomba endelea kunilinda Edina."

Machozi yalianza kumdondoka Edina. Pamoja na yote, bado alibaki kuwa mwanamke.

Mwanamke ambaye anapopata matatizo, au kupitia mambo magumu alihitaji faraja na mtu na kumpa moyo.

Kadili alipeleka mikono yake kwenye mikono ya Edina. Akamnyanyua na kumkumbatia.

Edina alilaza shingo kwenye kichwa cha Kadili, machozi yalizidi kumiminika.

Kwa mara ya kwanza Kadili alikuwa ameukumbatia mwili mororo wa Edina. Harufu ya marashi yaliyotokea kwenye nguo aliyovaa yalimpeleka mbali.

> **"Nilipokubali niliona sasa utaendelea kuwa hai mtu wangu, kwani tayari nimempumbaza mama, nikaolewa na Dk. Kapilima kwa sherehe kubwa sana kama binti wa kitajiri na ilipoisha nikaanza maisha ya mke na mume.**

Hakuna aliyezungumza kitu kwa dakika tano. Kila mmoja mawazo yaliondoka hapo na kukumbuka mambo mbalimbali nyuma.

"Basi usilie Edina, haya yote ni maisha, na mimi nitakusaidia kadri ya uwezo wangu kuvuka hapa ulipo. Japo mimi sina uwezo wa kipesa, lakini hata wa mawazo tu nitakusaidia."

"Najua najua, Kadili, najua kila kitu. Najua maisha yako, najua familia yako, nachotaka kutoka kwako ni kampani tu, mengine niachie rafiki yangu."

Baada ya kuridhika kukumbatiana, Kadili alirejea kwenye kiti chake na Edina aliendelea kukaa pale alopokuwa awali.

Bado Kadili kuna vitu vilikuwa vinamkereketa. "Niambie Edina, kifo cha mama nacho ni kweli kimetokea kwa sababu ya wewe kumkimbia mume, au maneno tu?"

Alionekana kufikiria kidogo. "Kuna asilimia fulani ya ukweli, kwa sababu mama alifariki siku mbili baada ya mimi kumtoroka mume. Kwanza kabisa mama alikuwa na matatizo ya moyo. Alikuwa na ugonjwa huo kwa muda mrefu na alikuwa anatumia vidonge ambavyo alikuwa akinywa kila baada ya muda fulani au anapohisi hali fulani si nzuri kwenye mwili wake. Nilipofuatilia baadaye niliambiwa kuwa alipata na mshtuko aliposikia mimi nimetoroka kwa mume na kikubwa zaidi ni kwamba sikurudi nyumbani. Na sikurudi kwa makusudi kwa sababu nilikosa ushahidi, mwanzo nilikwambia nilitaka ushahidi niupeleke kwa mama kuwa yule hakuwa mume mwema, lakini nilinyang'anywa ushahidi wa picha za video, unarudije nyumbani, unamwambije mama kuwa nimeondoka kwa mume bila maelezo ya kutosha, hasa ikizingatia kuwa anajua kuwa nimeolewa kwa shinikizo?"

**Itaendelea Jumamosi**

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA /MASHAMBA

**KIWANJA KINAUZWA**

KIPO CHANIKA BUYUNI PLOT 256, SQM 947 BLOCK 14. HATI IPO BEI NI SHILINGI MILIONI 14. KWA MAWASILIANO: 0743 113 138 / 0757 305 222.

## KAZI /AJIRA


**Nafasi za kazi** ualimu masomo ya sst/diploma 0656490706/0784142792


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA CHETI



**MACHELE ALBINUS**

anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0323-260** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Lake Sekondari mwaka 1989.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DAR/MBA/RB/515379/2019.**

115538002

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MAULID IDDI TOSIRI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA NOAH yenye namba za usajili T 654 DCA .Chassis No.SR500106606.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
DOD/CHA/RB/504642/2019.

115538602

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**HAMAD NASSORO AMOUR** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya LAND ROVER 110 yenye namba za usajili T 479 AMA .Chassis No.SALLDHMC7BA, Ingine No. 2946590.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
DOD/DOD/RB/514955/2019.

115538502

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**OTHMAN CHRISTOPHER MSIGWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SUZUKI SAMRAI** yenye namba za usajili T 648 BJA .

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
DOD/DOD/RB/405882/2019

115538402


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223311**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa kati ya tarehe 30/11/2019 mpaka tarehe 3/12/2019 kampuni ya **BONITE BOTTLERS LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **SHIRI MATUNDA INDUSTRIAL AREA** kuelekea **HOLILI BORDER** kupitia **MOSHI MJINI** gari hilo lenye namba za usajili:

   Truck KBZ 903A
   Trailer ZD 4287

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 22 |
| Upana | - | mita | 3.1 |
| Kimo | - | mita | 3.6 |

3. Njia itakayotumika: **SHIRI MATUNDA INDUSTRIAL AREA hadi HOLILI BORDER** kupitia MOSHI MJINI.

   Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215538102


**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# STERLING

## KUWEKA REKODI YA MSHAHARA CITY

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER City inataka kumfanya Raheem Sterling kuwa mchezaji anayelipwa mshahara mkubwa zaidi, kwa sasa mshambuliaji huyo anapokea pauni 350,000 kwa wiki.

Kwa mujibu wa ESPN, makubaliano ya awali baina ya mkurugenzi wa soka wa City, Txiki Begiristain, Ofisa Mratibu Mkuu, Omar Berrada na wakala wa Sterling, Aidy, Sterling atakuwa mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi kuliko wote kwenye klabu hiyo yenye maskani yake Etihad.

Wakati kwa sasa ikielezwa kwamba winga huyo raia wa England analipwa pauni 300,000 kwa wiki kutoka kwenye dili lake lile alilokubali mwaka mmoja uliopita ambalo linamfanya kubaki kwenye timu hiyo hadi 2023.

Katika kipindi hicho, Sterling alikuwa akishika namba mbili kwa nyota wanaolipwa fedha nyingi kwenye kikosi cha City, nyuma ya kiungo mshambuliaji Kevin De Bruyne, na sasa atalipwa pauni 450,000 kwa wiki kwenye mkataba huo mpya.



## MAJERUHI YA FABINHO YAMUUMIZA KICHWA KLOPP

**LIVERPOOL, England**

MAJERAHA ya kiungo wa Liverpool, Fabinho yameleta hofu kwa kocha Jurgen Klopp na mashabiki wake.

Fabinho aliumia wakati Liverpool ikitoka sare ya 1-1 na Napoli kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumatano.

Fabinho ambaye ni raia wa Brazil amekosa mechi moja tu ya Liverpool msimu huu katika Ligi Kuu England na ameibuka kuwa mchezaji muhimu katika eneo la kiungo baada ya kuanza kwa kusuasua katika soka la England.

Alitolewa uwanjani na nafasi yake kuchukuliwa na kiungo mwenzake, Georginio Wijnaldum katika dakika ya 19 na tayari anatazamiwa kulikosa pambano la leo Jumamosi dhidi ya Brighton kutokana na kuwa na kadi nyingi za njano, lakini wasiwasi mkubwa zaidi ni pambano la watani wa jadi dhidi ya Everton Jumatano usiku.

Klopp alielezea wasiwasi wake kwa majeraha ya staa huyo aliyemnunua kutoka Monaco misimu miwili iliyopita huku wakieleza kwamba atazamwe zaidi.

“Kitu kikubwa katika mechi ya leo (Jumatano) ni majeraha ya Fabinho. Ni kitu kikubwa. Ni mapema na wote tuna matumaini kwamba huenda hajaumia sana lakini amesikia maumivu makubwa,” alisema Klopp.

Alipoulizwa majeraha yake yanaweza kuwa makubwa kiasi gani, Klopp alijibu kwa kusema: “Sitaki kusema ninachotazamiwa kwa sababu ni matumaini huenda yasiwe majeraha makubwa.

Mara baada ya pambano hilo, Fabinho aliposti picha katika mitandao akiwa na staa wa zamani wa kimataifa wa Ureno mzaliwa wa Brazil, Deco huku akionekana akiwa amevaa kiatu maalumu cha kuulinda mguu wake.




## HAZARD KUIWAHI EL CLASICO

**MADRID, Hispania**

NYOTA wa Real Madrid, Eden Hazard ameshusha presha ya mashabiki baada ya jopo la madaktari kueleza kuwa hana majeraha ya kutisha na anaweza kuwahi kurudi uwanjani kwenye mchezo dhidi ya Barcelona maarufu kama El Clasico.

Hazard aliumia kifundo cha mguu hivi karibuni katika mchezo uliopita dhidi ya PSG kwenye mashindano Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Taarifa za madaktari zinaeleza kuwa anaweza kuwa nje kwa siku 10 tu kisha akarejea uwanjani.

Kwa siku hizo 10 upo uwezekano akaiwahi mechi kali dhidi ya Barcelona ‘El Clasico’ inayotarajiwa kupigwa Desemba 18 mwaka huu.

Hazard tangu atue Real Madrid akitokea kule Chelsea, hajawa kwenye kiwango cha kuvutia, huku akikumbwa na majeruhi ya mara kwa mara.



## HABARI MICHEZO



# HATIMAYE

## EMERY AFUKUZWA ARSENAL

**LONDON, England**

KOCHA Unai Emery amefukuzwa kuifundisha Arsenal ikiwa ni miezi 18 imepita tangu atue klabuni hapo.

Mhispania huyo, ambaye aliiongoza Paris St-Germain kutwaa taji la Ligi Kuu Ufaransa na kushinda makombe matatu ya Ligi ya Europa akiwa na Sevilla, alitua katika kikosi hicho cha Gunners Mei mwaka jana, akirithi mikoba ya Arsene Wenger.

Baada ya kutimuliwa jana, nafasi yake sasa itashikiliwa na aliyekuwa msaidizi wake, kiungo wa zamani wa Arsenal, Freddie Ljungberg.

Arsenal imesema kuwa imechukua uamuzi huo kutokana na matokeo yasiyoridhisha na kiwango cha chini kilichoonyesha na timu hiyo".

Timu hiyo imeshindwa kupata ushindi katika mechi zake saba zilizopita na ikipoteza kwa kufungwa mabao 2-1 ikiwa nyumbani dhidi ya Eintracht Frankfurt, katika mechi ya Ligi ya Europa iliyochezwa Jumanne iliyopita.

Ni matokeo mabaya zaidi kwa timu hiyo kukosa ushindi tangu Februari 1992, ikiwa ni mechi nane chini ya George Graham.

Na haijapata ushindi hata mmoja katika mechi za Ligi Kuu England tangu Oktoba 6 mwaka huu na wako pointi nane nyuma na timu zilizoshika nafasi nne za juu kwenye ligi hiyo.

Ljungberg aliongoza mazoezi ya timu hiyo jana na taarifa iliyotolewa na mabosi wa klabu hiyo iliongeza kuwa: "Tunamwamini kwa kiwango kikubwa Freddie atatupeleka mbele.

"Mchakato kwa ajili ya kusaka kocha mpya umeshaanza na tutatangaza hivi karibuni baada ya kukamilika."

Jumatano wiki hii, BBC Sport, ilitangaza kuwa Arsenal imemtaja Kocha Mkuu wa Wolves, Nuno Espirito Santo, kuwa yuko kwenye nafasi nzuri ya kuchukua mikoba ya Emery.

Makocha wengine wanaotajwa wanaweza kutua klabuni hapo ni pamoja na Kocha wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino, Kocha Msaidizi wa Manchester City, Mikel Arteta, Kocha wa zamani wa Juventus, Massimiliano Allegri na Kocha wa Bournemouth, Eddie Howe.

Chini ya Emery, klabu hiyo ilitajwa kutumia zaidi ya pauni milioni 130 kusajili wachezaji wapya akiwamo kiungo, Dani Ceballos kutoka Real Madrid, lakini kikosi hicho kilishindwa kupata matokeo mazuri.

Mechi ya mwisho ya Ligi Kuu England kupata ushindi ilikuwa ni dhidi ya Bournemouth, ambayo ilimalizika kwa kupata goli 1-0.

## Woodward asema alizuia usajili wa Mourinho



**MANCHESTER, England**

ED Woodward amekiri kuzuia usajili wa wachezaji wawili au mmoja aliowataka kocha Jose Mourinho wakati alipokuwa kwenye kikosi cha Manchester United, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

Mounrinho ambaye alitimuliwa Desemba mwaka japa pale Old Trafford sasa amepewa mikoba ya kuinoa Tottenham Hotspur.

Woodward, ambaye ni Makamu Mwenyekiti Mtendaji wa United alimfuta kazi Mourinho baada ya kuona timu haina mwendo mzuri licha ya timu kutumia zaidi ya pauni milioni 400 kusajili nyota wapya.

Woodward amesema: "Ni kweki kwamba kulikuwa na tofauti kidogo katika makubaliano ya mchezaji mmoja au wawili.

"Wakati mwingine mimi ndiye ninayepaswa kusema hapana, kwa sababu ni jambo la kawaida kwa kocha wetu kupingana na hilo, lakini tumekuwa tukisikiliza ushauri pia kwenye kusajili."

Mourinho alihitaji kufanya usajili wa beki wa kati akiwa United na aliwakosa Toby Alderweireld wa Tottenham, Diego Godin kutoka Atletico Madrid na nyota wa Bayern Munich, Jerome Boateng kabla ya klabu hiyo kutumia pauni milioni 80 kumnasa Maguire.

Mourinho alihitaji wachezaji wengi zaidi kutinga kwenye kikosi chake, lakini bosi wake hakuwa tayari kufanya hivyo katika dirisha la majira ya kiangazi la mwaka 2018 kabla ya kwenda kufukuzwa kazi ilipofika Desemba.

## Marcelo: Neymar wewe ni bora zaidi

**MADRID, Hispania**

MARCELO amemwambia Neymar kuwa yeye ni mchezaji bora kuliko Kylian Mbappe baada ya kuona Mbrazili mwenzake huyo akiwekwa benchi kwenye mechi dhidi ya Real Madrid ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa Jumanne iliyopita.

Real Madrid walicheza na Paris Saint-Germain pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu, lakini Neymar alikaa benchi na Mbappe akianza katika mchezo huo uliomalizika kwa sare ya mabao 2-2.

Baada ya mchezo huo, Marcelo alimwambia Neymar: "Unacheza vizuri kuliko Mbappe."

Mwanasoka huyo ghali duniani, Neymar aliingizwa kwenye kipindi cha pili wakati Real Madrid walikuwa mbele kwa bao la Karim Benzema.

Na mechi iliyoonekana kama vile Los Blancos wanakwenda kushinda baada ya Marcelo kumtengenezea bao la pili Benzema, dakika 10 kabla ya filimbi ya mwisho, PSG walisawazisha na wakatinga hatua ya mtoano wa timu 16.

Neymar alikaribia kabisa kuitema PSG kwenye dirisha lililopita la uhamisho wa wachezaji huku Real Madrid na Barcelona zikidaiwa ndizo timu zilizokuwa zikihaha kusumbukia huduma yake.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SANCHO RASMI AWEKWA SOKONI

Ni kutokana na mahusiano kati ya winga na klabu hiyo kuingia dosari...

**DORTMUND, Ujerumani**

MABOSI wa Klabu ya Borussia Dortmund wamesema kuwa wako tayari kupokea ofa kutoka sehemu mbalimbali kwa ajili ya kumuuza winga wa Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho, ambaye ana umri wa miaka 19, ifikapo mapema Januari, taarifa zinaeleza.

Kumekuwa na sintofahamu na mahusiano kati ya Sancho na Dortmund katika siku za hivi karibuni baada ya winga huyo kufanyiwa mabadiliko katika mchezo dhidi ya Bayern Munich.

Gazeti la The Independent liliandika kuwa nyota huyo alichelewa kufika katika kikao na mazoezi ya kuelekea mchezo dhidi ya Barcelona ambao ulichezwa Jumatano iliyopita na kumalizika kwa kufungwa magoli 3-1.

Sancho pia alisimamishwa na uongozi wa klabu hiyo mwezi uliopita, kutokana na kosa la kuchelewa kuripoti baada ya kumalizika kwa kalenda ya kimataifa, ambapo yeye alikuwa na kikosi cha England.

Kuna mawazo ambayo yameandikwa na wachambuzi mbalimbali ambayo yanaeleza kuwa " kuna vita ya pande zote mbili."

Inaelezwa kuwa imefika hatua Sancho anataka kuondoka na Dortmund wanataka kumuuza winga huyo.

Dortmund inaonekana kutoridhishwa na mwenendo wa wakala wa Sancho anavyolichukulia suala la uhamisho baada ya kuelezwa kwamba mchezaji huyo anaweza kuondoka katika kipindi cha majira ya joto.

Mbali na kuwapo na mchakato wa hatima ya winga huyo mwenye umri wa miaka 19, pia kuna suala lingine la uwezekano wa klabu hiyo kumtimua kocha wake, Lucien Favre, na mrithi wa nafasi yake itategemea hatima ya Sancho.

Lakini sasa wameamua kubadili uamuzi na kuwa tayari kupokea ofa ya kumuuza ifikapo Januari, huku tayari Manchester United na Liverpool zikitajwa kuwinda saini ya mchezaji huyo.

United walielezwa kuwa nafasi ya kumsajili Sancho katika kipindi cha majira ya joto mwaka jana isingewezekana, ambaye sasa amewekwa sokono na Liverpool ikijiandaa kumwania.

Klabu yake ya zamani ya Manchester City pia imeiambia Dortmund inamhitaji mchezaji huyo na ikiendelea kufuatilia mchakato wa Leroy Sane kutoka klabu ambaye anatakiwa na Bayern Munich.

Real Madrid pia imetajwa kumwania Sancho, ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 100, endapo ataondoka katika kipindi cha majira ya badiri.

## KWA UFUPI

**PELLEGRINI NJIA PANDA**

KOCHA wa West Ham United, Manuel Pellegrini, amebakiza mechi mbili ambazo zitaamua hatima ya nafasi yake kwenye timu hiyo baada ya kucheza michezo nane bila ya kupata ushindi. ***(Mail)***

**FABINHO AIVURUGA LIVERPOOL**

LIVERPOOL inahofia kumkosa kiungo wake Mbrazil, Fabinho (26), ambaye atakuwa nje ya uwanja kati ya wiki nne na sita kutokana na maumivu ya enka aliyopata katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Napoli iliyochezwa Jumatano iliyopita. ***(Mail)***

**SALZBURG YAIKANA LEIPZIG**

MKURUGENZI wa Michezo wa Red Bull Salzburg, Christoph Freund, amekanusha taarifa zinazoeleza kwamba RB Leipzig wamekaribia kukamilisha mchakato wa kumnasa straika wake raia wa Norway, Erling Braut Haaland (19), ambaye anahusishwa kuwindwa na Manchester United. ***(Bild - in German)***

**UNITED YABADILISHA GIA**

MABOSI wa Manchester United wamesitisha uamuzi wa kuwania saini ya straika wa Timu ya Taifa ya Croatia na Juventus, Mario Mandzukic, ambaye ana umri wa miaka 33. ***(The Athletic, via Inside Futbol)***

**MANDZUKIC, CAN SOKONI**

KLABU ya Borussia Dortmund imeweka wazi nia yake ya kumsajili straika wa Juventus, Mario Mandzukic na kiungo wa klabu hiyo na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Emre Can (25), katika usajili wa dirisha dogo la Januari. ***(Sun)***

**SPURS YAMGANDA FERNANDES**

NYOTA anayetakiwa na Tottenham Hotspur, Bruno Fernandes, anaweza kuondoka Sporting Lisbon, licha ya kusaini mkataba mpya ambao utamfanya auzwe kwa dau la pauni milioni 85. Katika mkataba wake inatajwa pia, Mreno huyo anaweza kuondoka kama itatolewa ofa ya kuanzia pauni milioni 60. ***(Mail)***

**MBAPPE KUTUA MADRID**

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Ufaransa ambaye alikuwa kwenye kikosi kilichoshinda taji la Kombe la Dunia, Kylian Mbappe (20), anatarajia kujiunga na Real Madrid. ***(Le Parisien - in French)***

**DEMIRAL ANUKIA MILAN**

AC Milan inajipanga kumsajili beki wa Juventus na Timu ya Taifa ya Uturuki, Merih Demiral (21), ambaye anahusishwa pia kuwindwa na Manchester City na Arsenal. ***(Calciomercato)***

**ARSENAL YAMFUATA RODRIGUEZ**

ARSENAL inajipanga kuwasilia ofa ya pauni milioni 35 ili kumnasa kiungo wa Timu ya Taifa ya Colombia na Real Madrid, James Rodriguez, ambaye anaamini anaweza kujiunga na Inter Milan au Paris St-Germain. ***(Eldesmarque - in Spanish)***

**VALVERDE AJIUNGA MADRID**

KIUNGO wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Uruguay, Fede Valverde (21), amesaini mkataba mpya na klabu hiyo ambao utamalizika ifikapo mwaka 2025 na endapo klabu nyingine itamhitaji, italazimika kulipa dau la pauni milioni 640. ***(Marca)***

**LJUNGBERG APEWA MIKOBA**

KOCHA Msaidizi wa Arsenal, Freddie Ljungberg, anatarajiwa kuongoza kikosi hicho kama klabu itafikia uamuzi wa kumtimua Unai Emery. ***(Times - subscription required)***

HABARI MICHEZO

# SIMBA YAENDELEA KUJIIMARISHA BARA

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba kimeendelea kujiimarisha kwa ajili ya mchezo wake unaofuata wa ligi hiyo dhidi ya Ndanda FC kutoka mkoani Mtwara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Dennis Kitambi, alisema kuwa anafurahi kuona wachezaji wake wanafuata kwa kiasi kikubwa maelekezo anayowapa katika mazoezi hayo.

"Nashukuru vijana (wachezaji) wanafuata kwa umakini mafundisho yangu, wanaelewa kwa kiasi kikubwa, hali ambayo inanipa matumaini," alisema Kitambi.

Kocha huyo alisema kuwa wachezaji wote wapo katika hali nzuri na kwa muda ambao atawaongoza, atahakikisha wanazidi kuimarika na kuja kupata matokeo chanya kwenye mechi za mashindano yote watakayocheza.

"Hali za wachezaji zinaendelea vizuri na kuimarika kila siku, kila mchezaji ana lengo la kuipa mafanikio klabu yetu, na tunaomba mashabiki wetu wazidishe ushirikiano," Kitambi alisema.

Aliongeza kuwa anaamini kikosi chake kitacheza mechi ya kirafiki ili kuongeza makali, lakini anasubiri kupata taarifa kutoka kwa uongozi wa klabu hiyo kufahamu maandalizi ya mchezo huo yalipofikia.

"Tutakua na mechi ya kirafiki, lakini mpaka sasa siwezi kuzungumza chochote mpaka pale nitakapopata maelekezo kutoka kwa viongozi wangu," alisema kocha huyo wa zamani wa Ndanda FC na Azam FC za hapa nchini.

Kitambi alipewa jukumu la kuinoa timu hiyo mara baada ya uongozi wa klabu hiyo kumsimamisha Mbelgiji Patrick Aussems ambaye anakabiliwa na kesi inayoendeshwa katika na Kamati ya Maadili. Makocha mbalimbali wanaendelea kutajwa kutua klabuni hapo akiwamo nahodha na kiungo wa zamani wa timu hiyo, Suleiman Matola, ambaye kwa sasa anaiongoza Polisi Tanzania.



Beki wa Simba, Pascal Wawa (kushoto), akimtoka kiungo wa timu hiyo, Jonas Mkude katika mazoezi yaliyofanyika kwenye Uwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam jana. **PICHA NA JUMANNE JUMA**

# Shabiki Yanga ashinda M-BET

**Na Mwandishi Wetu**

MAMBO mazuri! Shabiki wa Yanga, Barcelona na Manchester City, Samson Mlembe (23), ameibuka mshindi wa zawadi ya Sh. milioni 76.2 baada ya kubashiri kwa usahihi mchezo wa Perfect 12 wa kampuni ya M-BET.

Msemaji wa Kampuni ya M-Bet Tanzania, David Malley, amesema kuwa Mlembe, ameshinda fedha hizo baada yakubashiri kwa usahihi mechi 12 za ligi mbalimbali duniani.

Malley alisema kuwa Mlembe ambaye ni mkazi wa Dodoma amekuwa mshindi wa tano kwa mwezi Novemba na zawadi hiyo aliyopata, inatarajiwa kubadili maisha yake.

Alisema kuwa M-BET inaendelea kuwa nyumba ya mabingwa kwa kutoa washindi wengi zaidi ambapo mpaka sasa wametumia zaidi ya Sh. milioni 700 kwa washindi na bonusi kwa mwezi huu peke yake.

"Tunazidi kuinua vipato kwa Watanzania, tumeweza kutoa zaidi ya mamilioni ya fedha kwa mwezi huu na kuwa kampuni pekee iliyoweza kutoa fedha nyingi kwa washindi," alisema Malley.

Naye Mlembe alisema kuwa hakuingiwa na hofu baada ya kupokea simu kutoka kwa Allen Mushi ambaye ameshuhudia mara kadhaa akikabidhi zawadi kwa washindi.

"Mpaka sasa sijapanga nitumie fedha hizi kwa mambo gani, ni fedha nyingi ambazo sikutegemea kuipata, nitakaa na wazazi wangu na kujua nini cha kufanya, kwa kweli siwezi kukurupuka," alisema Mlembe.

Aliongeza kuwa kuna biashara mbalimbali za kufanya, lakini lazima uweke mikakati na mipango sahihi kabla ya kuanza ili kujiepusha na janga la kupata hasara.

## Azam waipania JKT Tanzania

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kupata ushindi mnono katika mchezo wake uliopita, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Cheche, amesema anatarajia kuendelea kutoka "dozi" katika mchezo unaofuata dhidi ya JKT Tanzania utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Cheche, alisema kuwa kikosi kinaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya mtanange huo na kiko tayari kusaka matokeo chanya.

Hata hivyo, Cheche alisema kuwa mechi hiyo itakuwa ngumu na ya yenye ushindani kutokana na wapinzani wao kutokubali kupoteza mechi mbili mfululizo.

"Mchezo utakuwa mgumu na wenye ushindani, lakini kwa jinsi nilivyowapanga wachezaji wangu hakuna kitakachoharibika, ninaamini tutaendelea kuwafurahisha mashabiki wetu baada ya kurejea nyumbani," alisema Cheche.

Naye Ofisa Habari wa timu hiyo, Jaffer Idd, alisema kuwa wanatarajia kuufunga Uwanja wao wa Azam Complex, kwa muda wa mwezi mmoja ili kupisha ukarabati.

Kiongozi huyo alisema wameamua kufanya ukarabati huo ili kuimarisha ubora wa uwanja na kwa kuuendesha kwa kufuata kanuni na maagizo ya Fifa.

## Mabinti Bara kulipiza kisasi

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa timu ya wasichana ya umri chini ya miaka 17, Bakari Shime, amesema kuwa kikosi hicho kitakwenda Uganda kurekebisha "makosa" yaliyofanywa na dada zao kwenye mashindano ya Kombe la Chalenji yaliyomalizika Jumatatu iliyopita.

Yosso wa Bara ni moja kati ya nchi nane zinazotarajiwa kushiriki mashindano ya Chalenji ya wasichana (U-17), ambayo yanatarajiwa kufanyika kuanzia Desemba 7, mwaka huu katika mji wa Jinja, Uganda.

Shime aliliambia gazeti hili kuwa, kikosi chake kimefanya mazoezi kwa muda mrefu na wanatarajia kwenda kufanya vizuri katika michuano hiyo ambayo inachezwa kwa mara ya kwanza.

"Tumepangwa katika kundi la kawaida, ninaamini hii ni safari nyingine ya Tanzania kuweka rekodi, kwa kufanya vizuri kama ilivyokuwa kwa dada zao," alisema Shime.

Nchi nyingine zinazotarajiwa kuwania ubingwa wa michuano hiyo ni wenyeji Uganda, Burundi, Sudan, Sudan Kusini, Ethiopia, Kenya na Djibouti.

Michezo
Jumamosi Novemba 30, 2019
Nipashe



## Sancho rasmi awekwa sokoni

HABARI UK 30



Beki wa Manchester United, Ethan Laird (kulia), akipambana kuwania mpira na kiungo wa Astana, Abzal Beysebekov, katika mechi ya Kundi L ya Ligi ya Europa iliyochezwa juzi usiku. United ilifungwa mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA SC YAZIDI KUTAKATA BARA

●●●Ni baada ya kuichapa Alliance FC katika mchezo wake wa Ligi Kuu uliochezwa...

**Na Adam Fungamwango**

RAHA ya ushindi imeendelea kutawala Yanga, baada ya timu hiyo kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Alliance FC, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza.

Kwa matokeo hayo, Yanga imefikisha pointi 16 kwenye kibindo chake, ikiwa imecheza mechi saba, kushinda tano, imepoteza moja na sare moja na kupanda nafasi tatu kutoka ya 15 hadi ya 12 katika msimamo wa ligi hiyo inayoongozwa na mabingwa watetezi, Simba.

Haikuwa mechi rahisi kwa Yanga kama ilivyotegemewa baada ya Alliance FC iliyotoka kufungwa mabao 5-0 katika mechi iliyochezwa Jumanne iliyopita kwenye Uwanja wa Nyamagana, lakini wenyeji hao walionekana kupania vilivyo licha ya udhaifu mkubwa waliyokuwa nayo.

Mnyarwanda Patrick Sibomana aliiandikia Yanga bao la kwanza dakika ya 25 baada mabeki wa Alliance kuuokoa mpira kizembe na kumkuta mfungaji huyo aliyepiga shuti la chini chini na kujaa wavuni na kumuacha kipa, Andrew Ntala, asijue la kufanya langoni kwake.

Mechi hiyo ilichangamka zaidi katika kipindi cha pili na dakika ya 54, Alliance ilipata bao la kusawazisha kupitia kwa Juma Nyangi ambaye alikuwa anacheza mechi yake ya kwanza baada ya kumaliza adhabu yake ya utovu wa nidhamu.

Nyangi aligongeana na wenzake kabla ya kuachia shuti kali ya juu lililompita kichwani kipa Mkenya Farouk Shikalo na kujaa wavuni.

Makosa ya mabeki wa Alliance, yaliisaidia Yanga kuandika bao la ushindi kupitia kwa David Molinga, aliyekuwa amezungukwa kwa mabeki wanne, lakini walimkaba kwa macho, akageuka mara mbili kabla ya kupiga shuti dhaifu, lakini lenye malengo lililowapita mabeki na kipa wao waliobaki kulaumiana.

Yanga ilianza pambano kwa kasi na sekunde ya 55 tu, ambapo Molinga alikaribia kufunga bao la mapema baada ya kuunganisha kwa kichwa mpira wa faulo kutoka kwa Juma Abdul, lakini shuti hilo halikuzaa matunda. Mpira wa kichwa ulipigwa na Ally Sonso ulitoka juu ya lango la Alliance baada ya kutokea kizaazaa langoni, kufuatia kona iliyochongwa na Abdul.

Alliance ilizinduka dakika ya 10, baada ya David Richard kuambaa na mpira kwenye wingi ya kushoto na kupiga krosi iliyopigwa kichwa na Heri Mohamed, lakini mpira ulipita pembeni kidogo mwa lango.

Richard aliikosesha Alliance bao la wazi alipobaki akitazamana na Shikalo, lakini alipiga shuti kubwa lililopaa juu la lango.

Matokeo ya mechi nyingine ya ligi hiyo iliyochezwa leo ilimalizika kwa wageni Ndanda FC kulazimisha sare ya bila kufungana na wenyeji Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

## Manula arejeshwa Stars ya Chalenji

**Na Mwandishi Wetu**

GOLIKIPA chaguo la kwanza wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Aishi Manula, ameitwa katika kikosi cha Timu ya Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars), ambacho kinatarajia kushiriki katika mashindano ya Kombe la Chalenji yanayotarajiwa kufanyika kuanzia Desemba 7 hadi 19 mwaka huu jijini Kampala, Uganda.

Manula aliachwa katika kikosi cha Taifa Stars, baada ya kumweleza Kocha Mkuu, Etienne Ndayiragije, kuwa anahitaji muda wa kupona majeraha yaliyokuwa yanamsumbua baada ya kumalizika kwa fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon 2019), zilizofanyika Juni mwaka huu.

Hata hivyo, Ndayiragije, amemwacha nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, kwa ajili ya kutoa nafasi ya kuwaandaa wachezaji wengine ambao atawatumia kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) zitakazofanyika Aprili mwakani.

Kikosi kamili cha Kilimanjaro Stars kilichoitwa kwa ajili wa mashindano hayo ni pamoja na Juma Metacha (Yanga), Juma Kaseja (KMC), David Kisu (Gor Mahia), Salum Kimenya (Prisons), Juma Abdul (Yanga), Nickson Kibabage (Difaa El Jadid) ,Mwaita Gereza (Kagera Sugar), Abdulimajid Mangalo (Biashara United), Fred Tangalu (Lipuli) na Kikoti Lucas (Namungo).

Wachezaji wengine ni Yussuf Mhilu (Kagera Sugar), Eliud Ambokile (TP Mazembe), Paul Nonga (Lipuli), Mkandala Cleophace (Tz Prisons) na Zawadi Mauya (Kagera Sugar), Bakari Mwamnyeto (Coastal Union)Mohamed Hussein, Miraji Athuman, Jonas Mkude, Muzaru Yassin, Gadiel Michael na Hassan Dilunga wa Simba, Shaaban Chilunda, Salum Abubakar "Sure Boy", Idd Seleman (Azam), Ditram Nchimbi (Polisi Tanzania), Keklvin John ( Football House) na Eliuther Mpepo wa Bulidco ya Zambia.

Kilimanjaro Stars imepangwa Kundi C pamoja na mabingwa watetezi Harambee Stars ya Kenya, Djiboti na "ndugu zao", Zanzibar Heroes.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >